# *UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU*

Bila shaka nimefurahi sana kuwaona wengi hivi wamekuja usiku wa leo, baada ya mimi kuwaweka hadi usiku wa manane jana. Sikufikiri nyote mngekuwa huku leo, lakini inaonekana kama mtakuja kwenye shule ya Jumapili, na hilo ni zuri sana.

2 Sasa tunasoma na kujaribu kuchukua tu wakati wetu juu ya Mafundisho haya ya kanisa. Nami ninalifundisha tu. Na sasa, kunaweza kuwa na wageni pamoja nasi, nisiowajua. Siko hapa maskanini vya kutosha kujua washiriki wa kanisa ni akina nani. Lakini nilikuwa nimetangaza kwamba hii itakuwa tu kwa washiriki wa kanisa. Kwa sababu, huko nje, watu wana mafundisho mengi sana mbalimbali, na kadhalika. Vema, na, wanaamini mambo hayo. Wamefundishwa kuyaamini. Na—na—halafu unapoingia katika kanisa lingine, labda, nalo linafundisha jambo lililo kinyume sana, vema, basi wanawazia, "Aisee, sikubaliani na Hilo." Mnaona? Vema, hatumaanishi kuwa wajuvi au kumdhuru mtu yeyote, sababu ya sisi kufanya hivi. Sasa, wewe amini chochote utakacho. Lakini sisi ni . . . Ninaweka hili, na sina budi kulisisitiza sana, kwa sababu inatubidi kulitilia mkazo. Haya ndiyo maskani inatetea, mnaona, kile tu tunachotetea hapa. Na, kwa njia hiyo, hatungependa ujisikie kuudhika na kufikiri kwamba tulikuwa tukijaribu kukudhuru katika imani yako, au kitu kama hicho. Hivyo sivyo kabisa. Na hii ni . . .

3 Tunapitia haya kila baada ya miaka miwili au mitatu, mahali hapa, na kile tunachotetea, fundisho tu, kile tunachotetea, na sababu ya kufanya hivyo. Kile, kwa nini tunaamini Hili. Na kwa hivyo ikiwa kuna wageni hapa ambao sio m—mshiriki wa hili kanisa, hakika tunafurahi kuwa pamoja nanyi mkiketi kwenye mjadala huu asubuhi ya leo na pia usiku wa leo.

4 Na, basi, Jumatano utaanza uamsho wa kawaida mkutanoni, ninamaanisha, maskanini hapa. Nami nimekuwa mbali kwa muda, kwenye mapumziko mafupi. Nilichoka sana, ikabidi niondoke, nipumzike kidogo. Na nimerudi hivi punde, najisikia vizuri, najisikia vema. Na kwa hiyo nitaondoka tena, mara tu huu utakapokwisha, wala sitarudi tena hadi Januari. Siendi mikutano yoyote; ninaondoka tu, kuendelea na mapumziko niliyokuwa nayo.

5 Lakini, tulipoingia, tulikuta kanisa likiwa na vurugu kidogo hapa na pale, na baadhi ya washiriki walikuwa wameanza kupata uvuguvugu kidogo, wakajiondoa, wakiwekeana uadui kidogo wao kwa wao, na kadhalika namna hiyo. Nilizunguka,

kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine, mpaka tukayatatua yote sasa. Ni sawa. Mnaona?

6 Wala hakuna kitu kibaya. Hakukuwako na kasoro yoyote kwa mfuasi yeyote. Wote ni wanaume na wanawake wazuri. Laiti wangeweza kutambua ya kwamba huyo ni ibilisi, anaingia kati ya watu. Hiyo ni kweli kabisa. Sio hao watu. Kama unaweza kumwacha ndugu aone jambo hilo, basi hataweka uadui dhidi ya jamaa huyo mwingine. Ana ninii . . . Ata—atajisikia vibaya. Atajisikia kama, "Naam, hiyo ni . . . Namsikitikia ndugu yangu." Mnaona, kama alifanya makosa, mbona, haikuwa ni huyo ndugu. Ibilisi ndiye aliyefanya hivyo.

7 Unasema, "Vema, jamaa huyu alifanya kitu *fulani, fulani*." Ndugu yako hakufanya hivyo; dada yako hakufanya hivyo; huyo alikuwa ni ibilisi aliyewaingia, aliyefanya hivyo. Kwa hiyo usimlaumu huyo ndugu, dada; mlaumu ibilisi, huyo ndiye aliyelisababisha.

8 Na kwa hiyo sasa katika Mafundisho haya ya kanisa, sasa, yanaweza kuwa ya kigeni sana kwenu. Yanaweza kuwa kwamba hutakubaliana nayo, hata kidogo. Lakini sisi tu . . . Hayo ndiyo tunayoamini. Tunayaamini kwa sababu yako katika Biblia, na tunayafundisha hivyo.

9 Sasa, jana usiku, somo letu lilikuwa: *Kwa Nini Sisi Si Madhehebu?* Sasa, sisi ni shirika kwa sababu sisi ni kanisa, lakini sisi si dhehebu. Halafu nilikuwa nikitoa sababu ya sisi kutokuwa dhehebu.

10 Sasa, tunapofungua huu mjadala asubuhi ya leo, kabla hatujafanya hivyo, hebu na tuombe.

11 Mungu Mpendwa, ni katika Uwepo Wako Mtakatifu ambamo tunakuja tena kuomba utakaso wa nia zetu wenyewe, nafsi zetu, tupate kujikabidhi Kwako kama chombo ambacho ungeweza kufanya kazi ndani yake, na kupitia kwake, kwa utukufu Wako mwenyewe. Na, Baba, safisha mawazo yangu, na nia yangu, na kunena kwangu, ili isiwe ni mimi ninayenena; lakini Roho Mtakatifu angeweza kuipaka midomo, na ya udongo, ili iweze kuleta Kweli ambazo Mungu Mwenyezi angelitaka Kanisa Lake lijue.

12 Nasi tungekuomba, basi, Bwana, kama ukifanya hivyo, kwamba ungeondoa kila pepo wa—wa matatizo, na kila pepo wa uadui na maovu, waondoke kwa watu, wapate kumsikia Roho Mtakatifu akinena, ili Mungu apokee utukufu kutokana na kukusanyika kwetu pamoja asubuhi ya leo. Na kama kuna jambo moja mioyoni mwetu ambalo haliko katika hali halisi, ambapo ungeweza kusema nasi, Ee Mungu, litupe mbali nasi, kama vile Mashariki ilivyo mbali na Magharibi. Kwa maana, tungejua tu mapenzi ya Mungu, kufanya. Kwa hiyo tuongoze kwa Roho Wako Mtakatifu, katika mjadala huu ujao juu ya Kanisa na Mafundisho Yake, na kile linachopaswa kutetea, na kwa nini

linapaswa kusimama hivyo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

13 Sasa, jana jioni tulikuwa tukitoa wa—wazo la ni kwa nini hatukuwa dhehebu lenye mpangilio. Nasi. . . Msingi kidogo tu kwa ajili ya hili. Ni kwa sababu tunaona, ya kwamba, katika dhehebu, linaweka kizuizi.

14 Sasa, tuna mambo mengi ya kujadili. Nasi tulilijadili, kwa nini hatukukubali wahudumu wanawake kanisani, jana usiku.

Na asubuhi ya leo tunataka, somo, ikiwezekana: *Ubatizo wa Roho Mtakatifu*, na ni kwa nini tunaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, na jinsi ubatizo wa Roho Mtakatifu unavyokuja, na yale ufanyayo, na jinsi unavyokufanya utende baadaye.

15 Halafu usiku wa leo, Bwana akipenda, nataka kuzungumza juu ya somo, "Uzao wa nyoka, wa hili katika siku hii." Sasa, watu hawaamini katika uzao wa nyoka, bali ni Maandiko. Mnaona? Sasa, bila kujali . . .

16 Sasa, hili, nikilititilia nguvu sana, silimaanishi sasa kwenu—kwenu ninyi wapendwa. Jambo pekee ninalojaribu kufanya ni kulipigilia, nasi tutalifanya kuwa gumu, mnaona. Kwa hivyo unapaswa kuongea kama . . . Ukisema, "Johnny, nenda uketi," anaweza asisikilize hilo. Lakini ukisema, "Johnny, keti!" Johnny atalizingatia zaidi. Kwa hivyo sasa tutapiga kelele, "Johnny, keti," asubuhi ya leo. Mnaona? Vema. Nataka kulizungumzia ili muweze kuelewa tunayomaanisha. Mnaona?

17 Na kama tukisema jambo ambalo ni kinyume na mawazo yako, na imani yako, sisi si kitu kimoja . . . Kumbuka, ya kwamba, katika kanisa hili likiwa lisilo na mipaka ya kimadhehebu, tunaamini ya kwamba Wabaptisti, Wamethodisti, Wapresbiteri, Mlutheri, Mkatoliki, Protestanti, Myahudi, chochote alicho, mradi tu yeye ni ndugu, yeye ni ndugu yetu, hivyo tu, haijalishi ni wa dhehebu gani. Mungu hatamwajibisha hilo, kuwa katika dhehebu.

18 Lakini, sababu za kuwepo na madhehebu. Sasa, hiki ndicho kinachoanzisha madhehebu. Mungu atafunua kitu fulani kidogo kwa mtu, nao watakuja na kuunda dhehebu kuzunguka imani hiyo waliyo nayo, ndipo Mungu hawezi kusonga mbele zaidi.

19 Methodisti ingewezaje kukubali chochote zaidi ya kazi ya pili ya neema? Walijiundia dhehebu chini ya hilo. Wabaptisti wangewezaje kuamini zaidi ya vile wao . . . "Wenye haki . . . " Au, Mlutheri, hasa, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Hicho ndicho walichoundia dhehebu. Wabaptisti wanawezaje kwenda mbali zaidi ya wanavyoenda? "Mbona, unapoamini, unampokea Roho Mtakatifu. Na kuzamishwa majini, na hilo latosha." Kwa nini? Hilo ndilo waliloundia dhehebu. Mnaona? Kwa nini Pentekoste inaamini, kwamba, "Unaponena kwa lugha, unaye Roho Mtakatifu, na hilo latosha"? Maana wamejiundia dhehebu

chini yake. Ndugu, mambo hayo yanaweza kuwa, kila moja, sawa, lakini Mungu hafungwi na maskini dhehebu lolote. Anasambaa tu juu ya kitu hicho chote, hivyo tu. Na—nasi tu—tunaamini hivyo.

20 Na hiyo ndiyo sababu kamwe hatufanyiki dhehebu. Bwana ametupa fursa ya kuunganisha kanisa hili dogo katika madhehebu mengi mbali mbali, lakini hatufanyi hivyo. Kwa sababu, tunataka kukaa jinsi hii ili tuweze kuwa chini ya utawala na uongozi wa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Lolote analotufunulia, nasi tunaona ya kwamba ni Kweli, na linaambatana na Neno Lake, huko nyuma kabisa na mbele katika Biblia, kwamba ni Kweli, na Roho anakubaliana nalo, hatuna vizuizi vya kimadhehebu vya kutuzuia kulikubali Hilo. Tunaliingilia moja kwa moja, na kusonga mbele.

21 Na kwa hiyo wakati dhehebu linaposema hivyo, kama church of Christ, wako chini ya dhehebu, linalojiita Church of Christ, kwamba, "Siku za miujiza zimepita, na mambo haya yote namna hiyo." Mbona, ungepata wapi jambo hilo katika Maandiko? Lakini hawangeweza kufanya lolote lingine juu yake. Wamejiundia dhehebu chini ya hilo, mnaona, kwa hiyo hakuna unachoweza kufanya juu yake.

Lakini tunataka kuwa huru, ambapo tunaweza kusonga tu jinsi Roho anavyotusogeza, kwa kilindi zaidi na kimo cha juu zaidi, nasi tunazidi kusonga mbele, zaidi, na zaidi, na zaidi, na zaidi, na zaidi kokote kule.

22 Lakini sasa hatutakubali ulokole wowote. Tunachora mstari papo hapo. Mtu akipata kitu kidogo ambacho Bwana amemfunulia, na hakipatani na Biblia hii, kote kote katika Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, linakuwa fundisho, basi hatutalikubali. Mnaona? Halina budi kutoka katika Biblia. Na haliwezi tu kuwa ni kwa ufunuo wa mtu fulani. Kama huo ufunuo upo pamoja na Neno, sawa.

23 Mtu mmoja alinijia, siku moja, naye akasema, "Nimekuja Marekani hivi punde, Ndugu Branham." Akasema, "Sasa, nikafahamiana na dada Mkristo, na," kasema, "dada huyu Mkristo alikuwa mmoja wa wanawake wazuri sana. Lakini," kasema, "wakaja kugundua kuwa alikuwa na waume watatu au wanne. Na," kasema, "kwamba—kwamba, wakati nimemfahamu, tangu nimekuwa hapa miezi mitatu, aliachana na huyo na kuolewa na mwingine." Kisha kasema, "Alikuwa na Roho Mtakatifu, alinena kwa lugha kabisa wakati wote, mara kwa mara, na," kasema, "alitoa unabii na ufunuo." Akasema, "Alikuwa mwanamke aliyejazwa na Roho kweli. Naye alikuwa mwanamke mhudumu." Kisha kasema, "Nilienda na nikamwuliza Bwana, 'Kwa nini liwepo jambo *fulani-fulani*? Kwa nini mwanamke huyu angeweza kufanya hivi?'" Kisha kasema, "Nikapata ndoto ya mke wangu. Na mke wangu

alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamume mwingine, ambao ulikuwa ni uzinzi. Halafu basi," kasema, "alikuja na kupiga magoti miguuni pangu na kusema, 'Je, utanisamehe nilichofanya?'" Akasema, "'Hakika, nimekusamehe.' Tena kasema, 'Kwa nini unanisamehe kirahisi hivi?' Kasema, 'Kwa sababu nakupenda.'" Kisha kasema, "Bwana akanena tena katika ndoto, akaniambia, kwamba, 'Hiyo ndiyo sababu ninamsamehe, ni kwa sababu ninampenda.'"

24 Nikasema, "Bwana, ndoto yako ilikuwa tamu sana. Ilikuwa nzuri sana, lakini Bwana hakukupa ndoto hiyo. Haiendani na Neno Lake." Hiyo ni kweli. Haitafanya kazi na Neno Lake. Haidhuru inaonekana kuwa halisi jinsi gani, haina budi kutoka kwenye Neno.

25 Katika Agano la Kale, wao walikuwa na njia tatu za kujua ujumbe. Ya kwanza, bila shaka, ilikuwa ni torati; ya pili, ilikuwa kwa nabii; nyingine, ni kwa mwotaji. Sasa, torati ilikuwa ni maandishi yaliyoandikwa yaliyowekwa ndani ya sanduku, na hizo zilikuwa ni zile amri na torati juu ya hizo amri. Na ndipo nabii aliweza kutabiri, ama mwotaji angeweza kuota ndoto. Ambapo, Mungu hushughulikia njia zote mbili, na manabii na ndoto. "Akiwapo mtu wa rohoni kwenu, au nabii, Mimi Bwana nitajidhihirisha kwake katika—katika—katika—katika ndoto, nami nitajidhihirisha kwake katika maono. Na ikiwa anayosema yatatimia, basi msikieni, kwa maana Mimi nipo pamoja naye. Yasipotimia, basi msimsikie."

26 Sasa, walipomchukua mtabiri, nabii, ama mwotaji, naye (wao) alikuwa na ndoto ama unabii, nao walitaka kujua kama hiyo ilikuwa ni kweli au la, walimpeleka kwenye kile kilichoitwa Urimu Thumimu.

27 Sasa, najua hilo linaweza kuwa, kwa baadhi—baadhi yenu, neno gumu kidogo. Lakini jambo ni kwamba, kwa kweli ilikuwa . . . Haruni akiwa kuhani mkuu juu ya yale ma—makabila kumi na mawili ya Israeli, alikuwa na mawe sita kila upande wa kifuko cha kifuani. Na kila jiwe lilikuwa jiwe la kuzaliwa la kabila, kama kabila la Yuda, kabila la Gadi, kabila la Rubeni, kabila la Benyamini. Kila moja lilikuwa na jiwe la kuzaliwa. Ndipo wakati lile jiwe la kuzaliwa . . . Lingekuwa linaning'inia kwenye moja ya mabamba kanisani, au mhimili. Ndipo walipomleta nabii huyu aliyekuwa na unabii ambao alisema Bwana atafanya jambo fulani, nao wakamleta hapa mbele, naye akasimulia unabii wake, ama akasimulia ndoto yake. Sasa, kama Mungu alikuwa katika ndoto hiyo ama katika unabii huo, taa hizo zilianza kuchanganyikana pamoja na kufanywa kama rangi ya upinde wa mvua ukiakisi jibu la Kimbinguni. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ukikubaliana na kila jiwe lililomo ndani, kila jiwe likichanganyisha sehemu yake, likiakisi tena pamoja na jibu la Mungu, "Mtu huyo ni nabii. Anasema ukweli." Au, "Ndoto hiyo ilitumwa na Mimi." Lakini kama

lilikaa bwete bila kusogea, sijali jinsi ilivyoonekana kuwa halisi, ilikuwa ni ya uwongo. Hawakuipokea.

28 Ni kielelezo kizuri jinsi gani siku hizi. Sasa, Urimu Thumimu ya Agano la Kale imeondolewa, kwa sababu ukuhani ulibadilishwa. Sasa Urimu Thumimu ni Neno la Mungu, Biblia. Naam, bwana. Hapa, Biblia ilisema, “Neno la kila mtu liwe uwongo, na Langu liwe kweli.” Na haidhuru inaonekana halisi jinsi gani mtu anapoisimulia, ama jinsi ndoto yake ilivyo halisi, ama ufunuo wake, kama, kila Kitabu katika Biblia, Biblia nzima, haiakisi nuru juu Yake, ya kwamba ni Kweli, achana nayo, achana nayo.

29 Sasa, unaweza kuchukua kipande kidogo cha Maandiko hapa, na kusema, “Yesu alifanya *hivi na hivi* nasi tunapaswa kufanya vivyo hivyo,” unaweza kulifanya liseme chochote unachotaka kulifanya liseme. Lakini halina budi kuja kote kote na kuafikiana kikamilifu na Neno la Mungu, ndipo basi ni kweli, huyo ni Mungu akisema hivyo. *Hii* ni Urimu Thumimu Yake.

30 Kwa hiyo, Mungu hajawahi, katika wakati wowote, kuwa na dhehebu la makanisa. Hebu niambie ilikuwa lini. Na, sasa, hakukuwako na dhehebu mpaka miaka mia tatu na sitini baada ya kifo cha mwanafunzi wa mwisho. Hilo lilikuwa ni kanisa Katoliki la Kirumi. Na kutoka kwa. . .Kanisa Katoliki la Kirumi, Mungu aliliita, katika Biblia, Ufunuo 17, “kahaba.” Huyo ni mwanamke mchafu. Na kutokana na hilo, alikuwa na binti, na hao binti walikuwa makahaba, wachafu kama alivyokuwa. Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema. Nalo kanisa Katoliki la Kirumi lilizaa Uprotestanti wote, nao wamerudi moja kwa moja na kufanya jambo lile lile alilofanya.

31 Na sababu ya yeye kuwa mchafu, alikuwa na kikombe cha mafundisho mkononi mwake, mvinyo ya ghadhabu yake ya uasherati wake. Naye akawanywesha wafalme wa dunia, naye akaketi juu ya “maji mengi,” na alitawala juu ya watawala wa duniani. Tuliona hilo kuwa hivyo katika Biblia. Tuliona ya kwamba alipaswa kuketi juu ya milima saba, kanisa. Tulipata hilo. Tuligundua kwamba alikuwa amepambwa kwa taji tatu: mamlaka ya kuzimu, mbinguni, na toharani. Kweli. Na mtawala wake alikuwa ni mtu; alikuwa mpinga Kristo, aliyeketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha kuwa yeye ni Mungu, akisamehe dhambi duniani. Tulikuwa na haya yote, tukayapitia na kuona kuwa ni kweli.

32 Kasema, “Hapa ni kwake yeye aliye na hekima.” Tunaona kwamba Roho aliendelea kusema waziwazi, “Kwake yeye aliye na hekima; kwake aliye na maarifa; kwake, roho mbalimbali, karama.” Je, hamwezi kuona Mungu akiliendeleza Kanisa hilo katika siku za mwisho? Hapana budi Kanisa lililojaa karama za kiroho litainuka, karama halisi za Mungu. “Hapa ni kwake aliye na hekima. Na aihesabu hesabu ya mnyama huyo, kwa maana ni

hesabu ya mwanadamu. Hesabu yake ni mia sita sitini na sita." Nasi tuliona mahali hapo palikuwa ni wapi, hasa. Isingeweza kuwa kamilifu zaidi. Iandike, wewe mwenyewe, "vicarivs," ambaye ni halifa wa Kristo, "filii" wa Mungu, VICARIVS FILII DEI, uone kama haitimii, katika herufi zako za Kirumi, uone kama huna mia sita sitini na sita. Angalia ikiwa haitaweka, sio juu ya kitu kingine ambacho kingekufanya ushuku *hili* au *lile*, bali mahali pale pale ambapo Maandiko mengine yote yanasema atakuwa ameketi.

33 Na sisi hapa, Waprotestanti, tukitoka moja kwa moja. Sasa, tunachojaribu kufanya leo ni kuleta na kuonyesha ya kwamba fundisho ambalo kanisa Katoliki lilileta, na limeleta, tumelikubali papa hapa katika kanisa la Kiprotestanti. Nasi tunawapa watu hilo, ambalo ni bilauri ile ile ya uasherati wa kiroho anaoutoa. Maana, si ya Kimaandiko. Ni ya kujibunia. Ni unabii wa uwongo. Ni uwongo. Ni ya ibilisi.

34 Ndipo tukagundua, kupata msingi kidogo, kuonyesha jambo hilo, wakati tunaoishi. Na tulilichukua jana usiku, kwamba, m—mtoto aliyezaliwa haramu, mtoto haramu, asingeweza hata kuingia katika mkutano wa Bwana kwa vizazi kumi na vinne. Hiyo ingekuwa miaka mia nne; miaka arobaini kwa kizazi kimoja. Jinsi dhambi ilivyokuwa ni ya kuchukiza! Ni ya kuchukiza jinsi gani, si ilikuwa, lakini jinsi ilivyo sasa. Na kama hiyo ilikuwa chini ya torati . . .

35 Naye Kristo alikuja kuikuza torati. Alisema, "Mmewasikia wakisema, wale wa zamani, 'Usiue'; lakini Mimi nawaambia, yeyote anayemkasirikia ndugu yake, bila sababu, amekwisha kuua." Aliikuza. "Mmewasikia wakisema, wale wa zamani, 'Usizini,' hilo lilikuwa tendo; lakini Mimi nawaambia, kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amefanya uzinzi." Aliikuza, mara elfu nyingi. Vema, kama ilichukua vizazi kumi na vinne kwa hilo kufifia, basi vipi wakati kioo cha kukuza cha Mungu kinapotupwa juu yake?

36 Na watu siku hizi, matineja huko nje katika shule ya upili, wakiwa na karamu za bia, na kunywa pombe, na kuishi . . . na wasichana wadogo wakiishi katika uzinzi, wavulana wadogo, na mambo kama hayo. Ni kizazi cha aina gani kinakuja baada ya hiki? Ni nini huwafanya wasichana hawa wadogo wafanye hivyo? Mama yao alikuwa kiruka njia, bibi yao alikuwa mwimbaji vilabuni. Naye alisema atawapatiliza watoto na watoto wa hao watoto uovu wa wazazi hadi kizazi cha tatu na cha nne. Unaweza kutarajia nini zaidi?

37 Na wakati mambo yote yanaanza kuvuja, nayo ile mbegu ya haki inaanza kukaa kando, ikipungua na kupungua. Na waovu wanaendelea tu, wa kidini sana, wanaendelea tu kuwa waovu zaidi, na waovu zaidi na zaidi, hakuna la kufanya ila kukiangamiza kitu hicho chote kama Yeye alivyofanya huko

nyuma katika uharibifu uliotangulia ile gharika. Kila wazo la mwanadamu daima limejaa dhambi. Kila kitu ambacho mwanadamu anafikiria siku hizi ni chupa ya wiski, ama mwanamke fulani, ama huko nje akikimbia huku na huko, hawawezi kuishi waaminifu kwa wake zao. Wavulana hawawezi kuishi wakweli kwa wasichana wao. Wasichana hawawezi kuishi wakweli kwa wavulana. Mbona, wamefikia mahali mpaka ibilisi amewafunga sana na kuwapagawisha na pepo wachafu, kitu hicho chote kimekuwa lundo la dhambi. Hiyo ndiyo sababu tuko kwenye hii siku. Na hiyo ndiyo sababu Urusi inacheza haswa mikononi mwa Mungu, kukitikisa kitu hiki kitoke hapa. Biblia inasema hivyo. Bila shaka. Mungu anatumia ukomunisti. Atautumia. Ukomunisti utaangamiza kitu hicho chote, kulingana na Maandiko, nasi tuko katika siku hiyo.

38 Sasa, kuleta mambo haya, mnaona. Sikilizeni, enyi watu, mnakabiliwa na hili. Nanyi, ni . . . Hii inaamua kikomo chako cha Milele, kwa hivyo usiichukulie kwa urahisi. Iangalie katika U—Urimu Thumimu inayoathiri, jinsi inavyoathiri Maneno.

39 Sasa, tunapozungumza juu ya mambo haya, uone kama yanaafikiana na Biblia, uangalie kama yanaendana na vile Maandiko yalivyosema.

40 Sasa, kila kanisa, kama msemavyo, "Mimi ni Mkristo." "Wewe ni wa dhehebu gani?" Hiyo inaleta tofauti gani, yeye ni wa dhehebu gani? Tunatambua ya kwamba dhehebu halina uhusiano wowote na Biblia ya Mungu. Na madhehebu yote ya Kiprotestanti ni makahaba. Biblia yako ilisema hivyo. Unaposema wewe ni Mmethodisti, wewe ni kahaba wa Kimethodisti. Ukisema wewe ni Mbaptisti, wewe ni kahaba wa Kibaptisti. Unaposema wewe ni Mpentekoste, wewe ni kahaba wa Kipentekoste. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Kwa hiyo, yeye ni, "Mama wa makahaba." Sasa, kama hayo tu ndiyo uliyo nayo . . .

41 Sasa, kama unashiriki katika dhehebu hili na bado wewe ni Mkristo, wewe ni Mkristo; nawe si Mmethodisti, wewe si Mbaptisti, wewe si Mpentekoste. Wewe ni Mkristo. Sio, mbona, hata . . .

42 Nilisikia mjadala asubuhi ya leo kwenye redio, nilipokuwa nikijiandaa kuja kanisani, kwenye mjadala huu wa Kikristo huko Louisville. Nayo makanisa yamechukua mtindo wa kuwafundisha watoto wao unywaji pombe wa kisasa.

Tutatoa kundi la wapumbavu wa namna gani? Ni kwa nini? Kwa sababu mama na baba zao nyumbani hawajui zaidi kuhusu Mungu kuliko vile Mhotentoti angejua kuhusu hekaya za Kimisri. Jiepushe na jambo hilo lote. Haikubidi kujifanya wa kisa- . . . kujifanya wa kisasa. Unafanya walevi sugu unapofanya hivyo. "Loo, tutamwacha msichana afanye *hivi*, na mvulana afanye *hivi*," na kadhalika namna hiyo. Unaweza kutarajia

nini? Hatuwezi kwenda kizazi kingine. Hatuwezi. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

43 Kwa hivyo, sitaki mnichukulie kama aina fulani ya tapeli. Huenda nikawa; kama ndivyo nilivyo, mimi ni kama tu . . . Mimi sijui hilo.

44 Nilimwambia mke wangu anayeketi pale. Nilisema, "Meda, kwani nimekuwa shupavu wa kidini? Je, nimerukwa na akili? Ama, ni Roho wa Mungu ambaye hawezi kustahimili mambo hayo, anayepiga kelele? Je, kuna kitu humu ndani ambacho kinanifanya hata niende kinyume na mawazo yangu, mapenzi yangu mwenyewe?" Nikasema, "Kuna mambo matatu tu inaweza kuwa. Inaweza kuwa ama nimerukwa na akili . . . " Iwapo nimerukwa na akili, sijui hilo. Mimi ni mtu mwenye wasiwasi, mtu mwenye fadhaa. Hiyo ni asili yangu tu. Karama yangu hufanya hivyo, lakini, kama mhudumu. Lakini mi— mimi . . . "Ama nimerukwa na akili, au nimekuwa mlokole, ama ni Roho wa Mungu." Ha—haina budi kuwa mojawapo ya mambo hayo.

45 Lakini, siwezi kustahimili kuona mambo hayo, na kitu fulani ndani kinapiga kelele tu. Na bado ninajua, kulingana na Biblia, ya kwamba haina budi kutukia. Basi kuna faida gani kupiga kelele? Mungu atasimamaje kwenye Hukumu na kukitupa kizazi hiki hapa juu kama hana sauti inayopiga kelele dhidi yake, kuleta hukumu? Mafarisayo watakuwa nini, kama hakungekuwako na Yohana wa kupiga mayowe kutoka nyikani? Itafaa nini, nikisema, "Hawapaswi kufanya *hivi*, na hawapaswi kufanya *hivi*, na hupaswi kufanya *hivi*, na hupaswi kufanya *hivi*. Na unapaswa kujazwa na Roho"?

Wanapitia hapo na kusema, "Amerukwa na akili! Kichaa! Kitu fulani kilimpata!"

Naam, kuna faida gani ya kulifanya? Kwa sababu, Mungu hana budi kuwa na sauti. Hatuna budi kuyasema, kwa vyovyote vile, ili aweze kuleta hukumu, aseme, "Ilikuwa hapo. Wewe si kwamba hujui habari zake." Hiyo ni kweli. Na usipopiga kelele, atafanya nini? Kuna kitu kinacholia, ndani yako. Huwezi kujizuia.

46 Sasa, sasa tunaona, basi, ya kwamba tulipoleta makala inayofuata tuliyo nayo hapa, kugundua, kwamba—kwamba, sababu ya sisi kutokuwa wa dhehebu. Nasi tunaamini kwamba kuna Wakristo waliozaliwa mara ya pili, watu watakatifu, katika Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, na kadhalika. Tunaamini ya kwamba Kanisa la Mungu ndilo Mbegu hiyo iliyochanganywa kote katika milki hii mpaka hapa, nalo linaingia kwa yale tuliyozungumzia jana usiku, nasi tutalijadili zaidi, kuchaguliwa tangu zamani. Si kwamba Mungu huamua awali chochote kiwe, bali, kwa kujua tangu

zamani Yeye anaweza kuchagua tangu zamani, kwa maana Yeye alijua mambo yote.

47 Nasi tuligundua jana usiku kuwa hakuna mtu aliyewahi kuokolewa, kama usiku wa leo, na majina yao yakaandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Jina lako ama liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ulimwengu haujaanza, au halikuwepo wala halitakuwepo. Tunaona, wakati Mungu alipomchinja Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wewe ulichinjwa pamoja na Mwana-Kondoo wako. Unaamini hilo? Tutaona katika dakika moja.

48 Hebu na tufungue Ufunuo, kuanza, Ufunuo 17 ama. . . Ufunuo 13:8, tuone hapa Biblia inasema nini juu yake ka— kama. . .wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa. Tuone kama alichinjwa katika mwaka wa 33 A.D., au 33 A.D., au kama ailichinjwa lini. . .wakati alipochinjwa. Vema. Sasa, hii ni Marekani katika unabii hapa, bila shaka. Sasa tunasoma hivi.

> *Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudia* (Nani? Yule mnyama.), *kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.*

49 Mwana-Kondoo alichinjwa lini, ati miaka elfu mbili iliyopita? Labda miaka milioni mia moja iliyopita. Kabla misingi ya ulimwengu haijawekwa, Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu. Loo, lakini sasa ninajisikia kubarikiwa. Kabla hapajakuwepo na ulimwengu, Yesu Kristo alikufa ili kuuokoa.

50 "Vema," unasema, "basi kwa nini Mungu, Mungu asiye na kikomo, akaruhusu dhambi?"

Unajua, kuna sifa katika Mungu. Na kama Mungu kamwe asingemruhusu Shetani. . .Alijua, alipomwumba Lusifa, ya kwamba yeye ndiye angeupotosha ulimwengu. Loo, Mungu wetu si kitu fulani kidogo, kilichosukumiwa kwenye kona moja, bali Yeye ni Mungu asiye na kikomo Ambaye hakuwa na mwanzo wala hatakuwa na mwisho. Na, ndani Yake, Yeye yuko katika sifa Zake. Yeye ni Mwokozi. Na angewezaje kujulikana kama Mwokozi kama hakungekuwa na kitu cha kuokoa? Tungejuaje. . .

51 Ni nani aliyekuwa wa kwanza? Wakati, ninauliza hilo swali. Ni nani aliyekuwa wa kwanza, Mwokozi au mwenye dhambi? Vema, ikiwa Mwokozi alikuwa wa kwanza, na Mwokozi ni mkubwa kuliko mwenye dhambi, je, mwenye dhambi alitokea wapi? Kama kusingekuwako na mwenye dhambi, hangalimjua kamwe kama Mwokozi. Ni yupi aliye na nguvu zaidi, mponyaji au mgonjwa? Mponyaji huchukua tu ugonjwa na kuuangamiza. Ni ipi ilikuwa ya kwanza, Mungu au kansa? Mbona, kulikuwako na Mungu, kwanza. Kwa nini akaruhusu u—ugonjwa basi?

Kwa sababu, kama anaweza kuuangamiza sasa, angaliufanya usitokee. Na kama Yeye hana kikomo, Yeye alijua ungetokea. Lakini basi, kama hafanyi hivyo—kama hafanyi hivyo, kama hakuna ugonjwa, basi asingejulikana kamwe kama Mponyaji. Lakini kwa kuwa Yeye ni Mponyaji, ilibidi kuwe na ugonjwa. Mnaona ninachomaanisha? Sasa, Yeye alijua mambo yote.

52 Sasa, katika Ufunuo 13:8, sikilizeni. "Naye Mwana-Kondoo alichinjwa" (Lini?) "kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Mungu katika nia yake isiyo na kikomo, akitazama chini kupitia mtiririko wa wakati, Naye aliona yale ambayo yangetukia, na jinsi ambavyo ingemlazimu kuumba na kushuka chini katika muda huu wa wakati, ili kudhihirisha hasa kile alichokuwa.

53 Kwa nini ninyi vijana . . . nyinyi wanaume mlio na wake zenu, mjaribu mwanamke na utaona aliumbwa kutokana na nini. Hiyo ni kweli. Mjaribu mwanamume, itatikisa chupa chini ya kinywa chake, ikiwa amekuwa mlevi sugu. Itakwambia kama aliokolewa kutoka kwayo au la. Ikiwa amekuwa mkorofi, mzururaji, mbwa mchafu anayevunja nyumba za wanaume wengine; mvue nguo mwanamke fulani na umfanye . . . umpitishe karibu naye, na itakwambia ameumbwa kutokana na nini. Hiyo ni kweli. Bila shaka.

54 Mungu, kuonyesha nguvu Zake, kuonyesha kile Yeye alichokuwa, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwokozi, alimruhusu mwenye dhambi kuwa hapa.

55 Kama nilivyosema, Malaika wataimbaje hadithi za ukombozi, wakati hata hawajui maana ya ukombozi? Lakini, tunaweza kuimba. Tunajua maana ya kupotea na maana ya kupatikana. Hujawahi kupotea, hujui maana ya kupatikana. Ni wale waliopotea, wanaojua maana yake. Ni wale ambao wamekuwa na ugonjwa, ndio wanajua jinsi ya kufurahia afya njema inapokuja. Ni yule mtu mwovu aliyetembea mitaani huko, ambaye hakuwahi kuwa na rafiki, wala kamwe hakuwa na mtu wa kuwakumbatia kwa mikono, wala kamwe hakuwa na mtu yeyote hata kuwaangalia na kuwazingatia; huyo ndiye mtu anayejua maana ya rafiki wa kweli, wa kumkumbatia. Hakika, huna budi kujua.

56 Tunawezaje kujua jinsi ya kuthamini mwanga huu wa jua, kama hakungekuwa na usiku? Ungejuaje kufurahia siku nzuri, angavu, kama kusingekuwa na siku ya mawingu? Ungejuaje kuthamini jua la joto la majira ya kiangazi, kama kusingekuwa na majira ya baridi kali? Sheria ya mema na mabaya. Ninaenda kando, kuhubiri. Simaanishi kufanya hivyo. Vema.

57 Ufunuo 17:8, ambapo sisi, kwa dakika moja tu sasa, kuonyesha sasa. Mwana-Kondoo alichinjwa lini? "Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Vema. Ufunuo 17:8.

> Naye *yule mnyama uliyemwona alikuwako, naye hayuko; naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu, na*

*kwenda kwenye uharibifu: nao hao wakaao* juu ya *nchi watastaajabu, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima tangu—kitabu cha uzima tangu* (lini?) *kuwekwa misingi ya ulimwengu, . . .*

58 Jina lako liliwekwa lini katika Kitabu cha Uzima? Kama nilivyosema jana usiku, mtu aliyeuandika ule wimbo, "Kuna jina jipya limeandikwa katika Utukufu, na ni langu, ni langu," kwa makusudio alikuwa sahihi, lakini Kimaandiko alikosea. Jina lako halikuandikwa usiku ule ulipomjia Kristo.

Yesu alisema, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Wala hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu. Wote wanijiao Mimi, nitawapa Uzima wa Milele, na kumfufua katika siku ya mwisho. Hakuna hata mmoja wao aliyepotea. Sipotezi chochote, maana hakuna mtu awezaye kuwapokonya kutoka katika mkono wa Baba Yangu, aliyewakabidhi Kwangu." Loo, jamani! Whiu! Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala hataingia kamwe hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hiyo ndiyo sababu kanisa hili linaamini katika usalama wa uvumilivu wa watakatifu, si katika mfano wa Kibaptisti, si katika mfano wa Kipresbiteri, bali katika mfano wa Biblia.

59 "Vema," unasema, "sasa, Ndugu Branham, nadhani ukiisha kuingia katika neema daima uko katika neema." Hiyo inaleta fedheha nyingi. Lakini mwanamume au mwanamke anapozaliwa kwa Roho wa Mungu, ya kale yamepita, mambo yote yamekuwa mapya, naye amezaliwa na kubarikiwa na Mungu wa Milele. Wala hawawezi kuangamia kama vile Mungu Mwenyewe asivyoweza kuangamia.

60 Je, unataka kuniambia kwamba Mungu, Mungu asiye na kikomo, angeshuka na kukupa Uzima wa Milele, akijua ya kwamba anaenda kukupoteza? Akuokoe hapa, akijua atakupoteza pale? Alikuokoa kwa sababu gani? Mbona, Yeye anajipinga Mwenyewe. Ikiwa alikuokoa wakati mmoja, umeokolewa Milele yote. Hakuna pepo kuzimuni wanaoweza kukuvuruga.

61 Sasa, ati Mungu asiye na kikomo Ambaye angeweza kujua mwisho tangu mwanzo, halafu akuokoe hapa, juma hili, huku akijua mwaka ujao utarudi nyuma, na akupoteze? Vema, anafanya kazi kama hiyo kwa sababu gani? Huo ungekuwa ni upumbavu; nisingefanya hivyo. Ikiwa ningekufanya kuwa rafiki yangu leo, nikijua utakuwa adui yangu kesho, vema, nisingefanya hivyo. Ningekuacha tu. Unaona? Mungu anakufanya mtumishi Wake, leo, kwa sababu Yeye anajua, na alijua kabla ya wewe kuja duniani. Wakati alipokuwa akitengeneza kalisi iliyoingia mwilini mwako, wakati alipoumba nurulimwengu ambayo wewe. . .iliyo ndani yako.

Wakati petroli na yote ambayo umeumbwa nayo, Mungu alipoiumba duniani, alijua kila nyuzinyuzi zako na kile ungefanya. Mungu asiye na kikomo anawezaje. . .

62 "Vema, afadhali nitembee kwa uangalifu leo; huenda nikarudi nyuma na kupotea kesho." Hukuwa umeokolewa hapo mwanzo. Huenda ikawa umechochewa, chini ya mihemko. Huenda ukafikiria tu kwamba umeokoka. Unaweza kujisikia kana kwamba umeokoka. Huenda ukaamini kwamba umeokoka. Huenda ukajiunga na kanisa. Huenda ukawa Mbaptisti mzuri, Mmethodisti, au Mpentekoste. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Jina lako daima. . .Kama ukiwahi kuokoka, uliokolewa kabla ulimwengu haujaanza, wakati Mungu alipomtuma Yesu, katika nia Yake, kumwokoa yule ambaye Yeye alimwona angeweza kuokolewa. Sasa, hataki kwamba yeyote aangamie. Hataki, lakini, kama Yeye ni Mungu, Yeye alijua ni nani ataangamia na ni nani hataangamia. Maandiko yanasema hivyo. Kwa hiyo haya basi.

63 Hiyo ndiyo sababu tunatofautiana na Baptisti, Wamethodisti, na wale wanaoitwa watu wenye mawazo ya Kikalvini. Lakini, Ukalvini ni wa kweli.

64 Kisha tutakuja upande wa Armenia. Walipata nini? Matendo. Hayo ni makundi ya utakatifu. Matendo, "Mungu asifiwe, nitaacha nywele zangu zikue," wanawake. Na, "Loo, Mungu asifiwe, hata sitavaa shati lenye mikono mifupi," mwanamume atafanya hivyo, na kadhalika namna hiyo. Hilo halina uhusiano wowote na Ufalme. Hapana, bwana. Unaweza kuacha nywele zako zikue ndefu, unaweza kuvaa nguo popote unapotaka, ama unaweza kufanya *hili*, *lile*, ama *linginelo*, na halitakuwa na uhusiano wowote nalo. Hujaokolewa kwa sababu ya nguo zako. Kama ni hivyo, Mungu angetengeneza tu mitindo fulani ya namna hiyo. Yesu hangelazimika kufa.

Umeokolewa kwa sababu Mungu alikuokoa, kwa neema, nawe unafanya mambo haya kwa kushukuru tu. Adabu ya kawaida itakwambia hivyo. Unafanya mambo hayo kwa kushukuru. Matendo ndiyo ninayomfanyia Mungu.

65 Kama sitahubiri mahubiri mengine, na kuishi hapa miaka mia moja na hamsini, ningali nimeokoka. Hakika. Sijaokoka kwa sababu mimi ni mhubiri. Nimeokolewa kwa sababu ni neema ya Mungu iliyoniokoa. Hakuna jambo moja ambalo ningeweza kufanya ili kuistahili.

66 Nimeshitakiwa kwenye sheria, sasa hivi, kwa kesi ya dola nusu milioni. Nao walisema, "Mbona, ulikwea huko. . .Hizo ni pesa ulizochukua huko nje, kulipia bili zako. Zilikuwa ni zako kabla hujalipa bili zako. Ukazipitisha kanisani mwako, lakini zilikuwa zako kwanza."

Nikasema, "Lakini sikuwahi kufanya jambo moja kwazo."

Kasema, "Naam, ulifanya," kasema, "uliwaambia kwamba utachukua sadaka ya upendo."

Nikasema, "Nataka mtu aniambie ilikuwa lini."

"Vema, unaomba kupitia kwa barua?"

Nikasema, "Tafuteni ofisini mwangu; si hata senti moja."

67 Mnajua, Biblia ilisema, "Msifikiri-fikiri mtakayosema, kwa maana mtapewa saa hiyo." Nami nilikuwa nimeketi pale karibu na hao mawakili wa serikali, na kila mmoja akinigombanisha, kutoka upande mmoja hadi mwingine; huku mimi sijui ABC zangu. Na pamoja na hao watu werevu ambao wamefunzwa kukufanya useme mambo ambayo kweli hukukusudia kuyasema, basi unawezaje kulinganisha akili na mtu kama huyo? Hawezi kamwe kulinganisha akili na Bwana wangu, hata hivyo. Maandiko haya yalisema, "Msifikiri-fikiri mnapopelekwa mbele ya wafalme na watawala."

Ninajua pesa nilizochukua huko, nilikuwa nimezitumia kwa ajili ya . . . Nao hawakukanusha hilo. Zilikuwa zimetumika kwa njia halali sana iwezekanavyo. Lakini wakasema, "Zilikuwa ni zako, kwanza, kisha ukazipeleka kwenye Maskani ya Branham."

Nikasema, "Lakini mimi ndiye mweka hazina wa Maskani ya Branham." Na hii . . .

Naam, akasema, "Sijui kuhusu hilo. Basi kwa nini wadhamini hawakufanya hili, lile, na linginelo?" Moja . . .

Nikasema, "Halafu mnaniita mdanganyifu?"

68 Kasema, "Tunadhani wewe ni mwaminifu sana." Kasema, "Ninataka kukuonyesha jambo fulani, Bw. Branham," wakili huyo.

Ninasema hivi kwa utukufu wa Mungu sasa, pekee, na hasa sana kwa vijana. Akasema, "Ninataka kuwaonyesha jambo fulani, kukuonyesha jinsi . . . " Ukiishi kulingana na Biblia, Mungu ataishi karibu na wewe. Na kama roho yako haikubaliani na kile Mungu anachosema, basi wewe huishi kulingana na Biblia.

69 Mnakumbuka jana usiku tulipozungumza kuhusu wahubiri wanawake, wanaposema, "Loo, ninaamini Roho Mtakatifu aliniita kuhubiri," na kadhalika namna hiyo? Biblia ilisema, "Mtu akijiona kwamba yeye ni nabii, au hata wa kiroho, na atambue kwamba Haya ni maagizo ya Bwana; lakini mtu akiwa ni mjinga, acheni tu awe mjinga." Basi unaposikia watu wakisema kuwa wanaamini katika wahubiri wanawake, inaonyesha ya kwamba hawako sawa na Mungu, ama hawaijui ile Kweli. Huo ndio Ukweli. Maandiko yanasema hivyo. Tulilipata Hapo, na linaafikiana kote katika Maandiko. Sasa, haijalishi jinsi inavyoonekana kuwa halisi, ni kinyume. Sio sahihi.

70 Sasa, tutapata kitu hapa sasa. Angalieni. Mwenyezi Mungu, Mungu asiye na kikomo, aliyeumba nchi, na mbingu, na alijua kila kitu, na alijua kabla ulimwengu haujaumbwa, kila kiroboto, kila nzi, kila kisubi, kila kitu ambacho kingepata kuwako. Nanyi mnaishi kwa Neno Lake.

71 Basi, nikisimama pale karibu na hao mawakili. Wakili huyu alienda pale na kusema, "Sisi kamwe, kwa vyovyote vile, hatujaribu kusema kwamba wewe si mwaminifu." Kasema, "Ulikuwa hujui kuwa mtu akikupa pesa zilikuwa ni zako kwanza." Kasema, "Ulitia sahihi hundi kutoka kwa Bw. Miner Arganbright, kutoka—kutoka California, ya Shirika la Wafanyabiashara Wakristo wa Full Gospel, ya elfu *kadhaa* za dola. Na siku iyo hiyo ukaitoa kwenye benki yako na kununua tikiti nne au tano za safari ya kwenda ng'ambo, karibu dola elfu ishirini na nne."

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Unadaiwa kodi ya mapato kwa hiyo."

Mbona, nikasema, "Tulisimama mumo humo kwenye benki iyo hiyo, naye akanipa ile hundi, nami nikaipa benki na kuziandika zile tiketi papo hapo."

Akasema, "Kama ulikuwa na hiyo hundi dakika moja," kasema, "nusu ya hiyo, ilikuwa ni yako. Ulikuwa nayo, nusu dakika. Ilikuwa ni yako, nusu dakika, kabla haijawa mali ya kanisa." Kasema, "Unadaiwa kodi ya mapato juu yake."

Kasema, "Alilipatia kanisa. Aliilipia ushuru wa mapato, na kulipa kanisa. Alikupa wewe."

Nami nikasema, "Unailipia kodi ya mapato, inaenda kanisani, ndipo haitozwi ushuru."

Kasema, "Hatutozi ushuru kanisa lako. Tunakutoza wewe."

Nikasema, basi, "Kwa nini," nikasema, "mtu yule yule aliyetia sahihi jina lake, ushuru wa mapato ya serikali, aliniambia nifanye hivi."

Akasema, "Hayuko na serikali tena."

Nikasema, "Walioandika Katiba hawapo tena na serikali, je, ingali inatumika?" Nikasema, "Siku moja hautakuwa serikalini tena, nawe unasema nini basi?" Nikasema, "Je, tunatumikia serikali ya aina gani?" Bila shaka.

Lakini, basi, naye huyo mtu mwingine akasema, "Bw. Branham," akasema, "tunaona hapa, ngoja nikuonyeshe kuwa tunajua kila senti uliyotumia iko wapi."

Nikasema, "Vema."

Akasema, "Hapa kuna mahali ambapo ulikuwa na mkutano Canada, huko Alberta, na huko ulipewa sadaka ya upendo ya dola elfu tatu."

Nikasema, "Naam, bwana."

Kisha kasema, "Jumapili iliyofuata. . .iliyotangulia, hiyo, hasa, ulitoka ukaona mahali palipokuwa na kanisa la kale, nao walikuwa wakiabudia katika kanisa hili, wala halikuwa na paa juu yake. Nawe ukawapa hao watu hizo dola elfu tatu, kujenga kanisa."

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

Kasema, "Lakini unadaiwa kodi ya mapato juu yake." Kasema, "Uliitoa kwa kanisa." Kasema, "Unaona, zilikuwa ni zako kabla hazijawa za kanisa."

Akasema, "Je, si ni kweli, kwamba mtu *fulani*. . ." Nami sitalitaja jina lake, maana wengi wenu mnamjua. "Nyumba yake iliteketea, humu nchini, nawe ulikuwa umeingia, kutoka kwenye mkutano wako, nawe ulikuwa na dola elfu moja mia tano." Sasa, hiyo inaweza kusikika kama pesa nyingi sana, kwa mmoja wenu nyote. Lakini hiyo ni siku kumi na tano tu kwangu kushughulika, au kupumzika. Inanigharimu zaidi ya dola mia moja kwa siku, kama ninahubiri ama sihubiri, kushughulikia ofisi na kadhalika. Kisha akasema, "Ulikuwa na dola elfu moja mia tano. Na mtu huyo alikuwa. . .nyumba iliteketea. Alikuwa na yapata watoto sita, nawe ukampa hizo dola elfu moja mia tano." Hakika, walikuwa na hundi yangu imewekwa hapa.

Nikasema, "Hiyo ni kweli." Nikasema, "Ungefanya nini, mtu mwenye watoto watano akiishi katika hema, na hali ya hewa ni sifuri na theluji juu ya nchi? Unafikiri ningeweza kukaa katika nyumba nzuri na kujua ya kwamba mtu huyo na hao watoto wadogo huko nje, wanaganda, na makoti yaliyojazwa karibu nao, huku nikiwa na pesa ambazo zingeweza kumsaidia?"

Akasema, "Je, si ni kweli kwamba mtu alikufa kwenye uchochoro hapa juu? Naye alitoka Kentucky. Hakuwa hata na pesa za ibada ya mazishi yake, nawe ukamzika mtu huyo. Nawe pamoja na mke wako mlichukua pesa na mkashuka kwa J. C. Penney." Mkazifungua hizo hundi. Kasema, "Mkatumia zaidi ya dola mia mbili kwa ajili ya nguo za watoto hao."

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

Akasema, "Si ni ukweli kwamba mwanamke mkongwe papa hapa katika jiji *fulani* hili. . ." Anayeishi, wakati huo, New Albany. Kisha kasema, "Ulimpa dola mia tatu na kitu, ili kulipa bili ya vyakula, ambapo, walikuwa wamemkatalia, juu yake. Kisha ukalipa karibu dola mia tano kwa ajili ya kodi yake ya nyumba, ambapo walikuwa wakitaka kumfukuza kwenye majira ya baridi kali. Nawe ukamlipia kodi ya—yake hadi Juni iliyofuata, na pia ukasimamia bili yake ya vyakula ambayo ilifikia dola elfu moja mia nne au elfu moja na mia tano tena."

Nikasema, "Nakumbuka hicho kisa vizuri. Mama mzee, mwenye umri wa miaka themanini, mwenye binti aliyeteseka, na mvulana mhubiri huko Georgia, anateswa na baridi yabisi, na

amelazwa kitandani, na hakuna msaada mwingine. Ungefanya nini kuhusu hilo?" Nikasema, "Naam, nilifanya."

Kasema, "Je, halmashauri yako ya wadhamini ilijua hili?"

Nikasema, "Hapana, bwana, hawakujua."

"Mkeo alijua hili?"

Nikasema, "Hapana, bwana, hakujua."

Kasema, "Basi kwa nini ulifanya hivyo?"

72 Nikasema, "Kwa sababu Bwana wangu alisema, 'Usiruhusu mkono wako wa kushoto ujue kile ambacho mkono wako wa kuume unafanya.'" Nikasema, "Je, mna sheria yoyote inayoshinda sheria za Mungu?"

Na papo hapo Roho Mtakatifu akaja kuokoa, vizuri sana jinsi afanyavyo. Unasema mambo, bila kujijua, bila kujua unayasema, ukimwacha tu Roho Mtakatifu azungumze.

Nikasema, "Vema, vema, ikiwa unadai kwamba nina deni hilo," nikasema, "nitafanya vizuri niwezavyo." Nikasema, "Mimi si mvulana tena, lakini nitajitahidi niwezavyo kuilipa." Nikasema, "Sina deni la mtu yeyote, nijuavyo mimi." Nimejaribu kuwa mkweli. Nimeingia kwenye deni ya maelfu ya dola, na ninailipa kwa dola moja kwa juma. Lakini, kwa neema ya Mungu, nimeilipa. Nikasema, "Ukidai na kunithibitishia kuwa ninadaiwa hizo pesa ninazowapa watu hao. . . " Nao wakaendelea kuonyesha mahali ambapo ni karibu dola elfu ishirini, katika miaka kumi iliyopita, nilitoa namna hiyo.

Naye akasema, "Wadhamini hawakujua lolote kuhusu hili."

Nikasema, "Hawakuhitajika wajue." Na hivyo akasema. . . Vema, kisha akasema. . .

73 Nikasema, "Kinachoniumiza, ni kujua ya kwamba wale wajane na mayatima maskini, watalazimika kuzilipia kodi ya mapato, pia, au wafe, wakidaiwa na serikali." Sikujua nilichokuwa nikisema. Huyo alikuwa ni Baba akinena, nami sikujua.

"Loo," akasema, "hapana, hawatalazimika kuzilipia kodi ya mapato."

Nikasema, "Kwa nini hawatalazimika kulipa?"

Kasema, "Unaona, hiyo ilikuwa zawadi isiyoombwa."

Ndipo Roho Mtakatifu akaniamsha. "Loo," nikasema, "kwani zawadi isiyoombwa haitozwi ushuru?"

Kasema, "Hiyo ni kweli."

Nikasema, "Basi sidaiwi chochote na serikali, kwa kuwa sikuwahi kuchukua sadaka maishani mwangu."

Ndipo wakili wangu akasimama, akasema, "Bw. Branham unaweza. . . "

Nikasema, "Ninaweza kuwapa barua milioni mbili huko Washington, kuthibitisha hilo." Nikasema, "Sikuwahi kuchukua sadaka."

Kasema, "Lakini unapotoka ukaenda kwenye mikutano hii, na pesa hizi ambazo zimechukuliwa na wahudumu hawa na kuilipia hii," kasema, "una namna fulani ya uelewano kwamba utapata kitu."

Nikasema, "Hata."

Akasema, "Basi, vema, hivi wewe huombi kupitia barua?"

Nikasema, "Hata."

Kasema, "Unapataje pesa zako?"

74 Nikasema, "Zile watu hunitumia." Ninatazama usoni mwa watu sasa hivi wanaonitumia zaka sikuzote. Sikuwahi kuwaomba. Wanatuma tu. Huyo ni Roho Mtakatifu. Ana uwezo wa kuwashughulikia walio Wake.

Naye akasema, "Vema, basi, Bw. Branham," kasema, "unaweza kuthibitisha hilo? Je, unaweza kunipatia barua kwa angalau miaka minane au kumi nyuma kwamba ulipokea matoleo bila kuomba?"

Nikasema, "Nyingi utakavyo."

Akasema, "Nataka tatu kwa kila mwaka."

Nikasema, "Sawa, utazipata."

Kasema, "Kisha utanipa ufunguo wako wa sanduku la posta, na uniruhusu. . . Uache barua zako zilundikane siku mbili au tatu, na kisha nishuke na kulifungua, mimi mwenyewe?"

Kasema, "Unaweza kufanya chochote utakacho. Unaweza kuja ofisini mwangu pia."

Akasema, "Wewe huomba pesa kwa njia gani?"

Nikasema, "Hakuna."

"Unatuma nini kwa barua?"

"Vitambaa vya maombi."

"Je, unavilipiza?"

75 Nikasema, "Njoo, usome barua ninazotuma pamoja navyo." Jambo lilikuwa hilo. Sasa naidai serikali kwa zote nilizolipa, kodi ya mapato, kwa miaka ishirini iliyopita. Mnaona?

"Usitafakari utakayosema, kwa maana si wewe unayesema, ni Baba aishiye ndani yako, anayesema." Unaona? Hiyo ndiyo sababu tunaamini katika kudumu na Neno. Huenda ikawa ni muda mrefu, lakini itafanya kazi sawasawa, kulingana na Neno.

76 Sasa, hiyo ndiyo sababu tunaamini kwamba Biblia inatwambia ya kwamba kabla ya ulimwengu kuumbwa, na kabla haujakuwako, kwamba Baba alimchinja Mwana-kondoo. Na ndipo alipomchinja Mwana-Kondoo, aliweka kila moja la

jina la watoto Wake wanaokuja katika Kitabu cha Uzima, na tunaishi tu kufikia wakati huo hadi yote yatakapomalizika. Unaona ninachomaanisha? Mungu asiye na kikomo alijua jambo hilo, ya kwamba kabla ulimwengu haujaanza aliona mpango wa kile ambacho kilipaswa kufanywa, Naye aliufanya tu.

77 Sasa kumbuka, kama Mjenzi Mkuu, Baba, wakati alipoumba ulimwengu huu na kuweka kalisi, potashi, na petroli, na vitu hivi vyote mbalimbali ambavyo hujumuika kuunda miili yetu, alijua kila sehemu yake na alijua ni aina gani ya umbo na mwili ambao ungekuwa nao kabla haujaumbwa. Bila shaka. Alijua kikomo chake cha Milele. Naye anajua ni roho wa namna gani wangekaa kwenye hii.

78 Na sasa, kabla hatujamaliza somo hilo, itabidi tulichukue usiku wa leo, katika "uzao wa nyoka" na katika "uzao wa mwanamke," na kulishusha na kuwaonyesha kwa nini mambo yako hivyo. Tuone jinsi uzao huo wa nyoka ulivyoshuka, jinsi uzao huo wa mwanamke ulivyoshuka; jinsi uzao huo wa nyoka ulivyoanza kutawala, kutawala, kuwa mkuu zaidi, na zaidi, zaidi, zaidi, zaidi, mpaka sasa hakuna kilichosalia ila masalia machache tu ya majina yamesalia, yaliyoandikwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

79 Lakini wakati huo Mwili umeumbwa, na hilo jina la mwisho lililo kwenye Kitabu litatambuliwa hapa duniani, Vitabu vinafungwa, kwa kuwa imekamilika, hadithi ya ukombozi imesomwa kikamilifu. Ndipo tutaenda kumwona na kukutana Naye katika ufufuo. "Yeye asikiaye maneno yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele na kamwe hatakuja Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

"Hakuna mtu anayeweza kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu." "Na si yeye apendaye wala yeye apigaye mbio; ni Mungu arehemuye," yalisema Maandiko.

Si yeye atakaye. Watu wengi husema, "Nitajiunga na kanisa. Nitakuwa mtu mzuri. Nitafanya *hivi*." Hilo halina uhusiano wowote nayo. Ni Mungu arehemuye.

80 Sasa, mnaona, wakati Mungu alipoanza, katika. . . Kuna Roho saba za Mungu, kama tu zile rangi saba katika upinde wa mvua. Na hivi umewahi kutambua? Kipande cha kioo chenye pembe tatu huakisi rangi saba kamili. Je, umewahi kujaribu hilo? Weka kipande cha kioo chenye pembe tatu; bado ni kipande kimoja tu cha kioo, lakini, katika pembe tatu, kitaakisi rangi saba. Hivyo ndivyo Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, wakiwa Mmoja, bado wanaakisi zile sifa saba za kiroho za Mungu.

81 Na, basi, Roho mkuu wa kwanza wa Mungu, ambaye ni upendo. Mungu, kama upinde mkuu wa mvua. Tusingeweza kuwazia jinsi anavyoonekana. Lakini tuseme tu kwamba anafanana na upinde wa mvua, hizo Roho. Roho kamili ya

upendo, *nyekundu*. *Samawati*, ile Roho kamili ya ushirika. Roho hizo zote kamilifu tu! Ndipo basi wanaanza kujishusha, wakishuka. Nao wakaja chini kabisa kutoka kwa u—upendo wa *filio* au. . . Upendo wa *Agapao*, hadi kwa upendo wa *filio*, na kushuka hata kwenye tamaa mbaya, na chini kwenye iliyo duni kabisa.

Ndipo Mungu Mwenyewe akawa Mwanadamu, Yesu, na akashuka chini kwa njia iyo hiyo, kwenye mashimo ya chini kabisa ya kuzimu, akawachagua wale aliowajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ambao majina yao yaliandikwa katika kile Kitabu, na kuwakomboa wamrudie Yeye. Haya basi. Hadithi ya ukombozi haiwezi kujulikana kikamilifu mpaka tutakapomwona na kusimama katika mfano Wake.

82 Sasa, hiyo ndiyo sababu sisi si madhehebu. Ndio maana hatushiri-. . . Tunashirikiana katika kila hatua tuwezayo, kwa ajili ya Mungu. Lakini ndio maana sisi si dhehebu. Sasa, kutoka katika madhehebu hutoka hayo mambo ya uwongo.

83 Sasa, kama nilivyosema, ninagonga kwa nguvu, kwa sababu ninataka lishikilie. Sasa, huko nje, katika kanisa la mtu mwingine, nisingewazia mambo haya. Ningekuwa Mkristo na ndugu vya kutosha kukaa tu kwenye kanuni kuu ambazo sote tunakubaliana juu yake. Mnaona? Lakini, ni—ni kama tu, hatutaki udanganyifu.

84 Nilikuwa nikizungumza na mvulana mdogo jana, ambapo nilikuwa nikiwinda kuchakulo, jana asubuhi, huko chini kabisa kwenye milima ya Kentucky. Wala sikuona lile bango dogo lililobandikwa msituni, nami nilikuwa nimeketi upande ule mwingine. Nami nilifikiri ilikuwa ni Ndugu Banks hapa, anayekuja kupitia msituni. Alikuwa akiwinda kuchakulo, pia, katika eneo lile lile. Ndipo nikamwona akija, nami nikampigia mbinja huyo kijana. Nilifikiri ilikuwa ni Ndugu Wood, amevaa kama yeye kabisa. Akageuka, nami nikaona siye.

Na Ndugu Wood alikuwa ameniambia ya kwamba kulikuwa na mahali huko juu palipotahadharishwa. Nami sikujua. Hakuna nyua za mpakani; misitu tu. Nami nitajuaje ni mti gani wa hikori ulio wa upande gani? Kwa hiyo nilikuwa nimeketi pale nikisikiliza kuchakulo wakibweka. Na nilikuwa nikiwazia, "Vema, sasa, usiku wa leo naenda nyumbani na kuanzisha mkutano. Ninarudi kazini tena." Ndipo mvua ikaanza kunyesha, na dhoruba kuvuma.

85 Nami nikamwona jamaa huyu, na nikazungumza naye. Nikaenda pale na kugundua kuwa nilikuwa kwenye eneo lake. Mnaona? Basi nikazungumza naye. Akasema, "Loo, hiyo ni sawa." Akasema, "Jamani, winda tu popote utakapo." Nami nikasema, vema. . . Akasema, "Hukuwa kwenye eneo langu. Ulikuwa umeketi mbele ya ule mti wa hikori." Kasema, "Upande huu wa hikori ndilo eneo langu. Lakini," asema,

"haijalishi, Ndugu Branham. Winda popote utakapo. Njoo hadi nyumbani. Baba angependa kukuona." Mnaona? Nami nikasema, "Vema . . . "

Tukaanza kuzungumza juu ya Biblia. Kisha wakati tukiwa kwenye mada ya uwindaji, alisema hivi, alisema, "Ndugu Branham, hakuna mtu hapa chini anamyejali mtu yeyote anayewinda. Lakini," kasema, "baba yangu alikuwa hapa nje siku moja na mwindaji fulani wa jiji akatoka na kumwua mmoja wa kondoo wake mwenye uzito wa kama ratili sitini au sabini, naye akampigia kelele jamaa huyo, naye huyo jamaa akamrushia risasi, kwa bunduki." Akasema, "Hiyo ndiyo inaufanya kuwa mbaya." Kasema, "Hatujali uwindaji."

86 Vema, hilo ndilo jambo lile lile ninalozungumzia. Sijali wewe ni wa dhehebu gani, bali kaa na Biblia na Roho Mtakatifu. Si dhehebu lako ambalo tuna wasiwasi nalo; hayana tofauti. Lakini, ni kudumu na Biblia au kukubali mafundisho ya sharti ya kujibunia. Dumu na Biblia.

87 Sasa, walileta dhehebu, ambalo lilikuwa ni makosa. Sasa, jambo la pili walilokuwa wameleta, ambalo lilikuwa ni kosa, lilikuwa ni ubatizo wa maji. Ubatizo wa maji, kama inavyofundishwa katika Biblia, ni kwa kuzamishwa. Lakini kanisa Katoliki lilileta kunyunyizia ama kumwagiliwa. Wala hakuna Maandiko katika Biblia yanayounga mkono kunyunyiziwa au kumwagiliwa; hakuna mahali kama hapo panapopatikana katika Biblia. Ni kwa kuzamishwa.

88 Vema, basi, lakini baadaye likaja, baada ya kanisa Katoliki, na kanisa la Kilutheri, pamoja na kumwagilia kwao. Na kisha likaja kanisa la Kianglikana, na kadhalika, wakati likishuka.

Ndipo, baada ya kitambo kidogo, Wabaptisti wakaingia na Wakampbeli, kurudi kwenye kuzamisha tena. Vema, Shetani aliliona hilo, kwa hiyo akawapa tu jina la uwongo la kuzamishia. Nao wakaanza kutumia Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Hakuna hata sehemu moja ya Maandiko katika Biblia ambapo mtu yeyote aliwahi kuzamishwa kwa jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Na yeyote anayefundisha hilo ni mwalimu wa uwongo. Nami niliwaambia nitaifanya ishikamane.

89 Sasa, kama huoni hiyo ni kweli, nataka swali lako kwenye jukwaa hili, likinionyesha. Kama unaweza kunionyesha mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa, katika Biblia, kwa jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," nitaweka alama mgongoni mwangu, kama "mhubiri wa uwongo," na kwenda huku na huko barabarani, nikilia kwa sauti yangu yote, huku nimeinua mikono yangu, "Mwalimu wa uwongo!"

Hakuna kitu kama hicho. Ilitoka wapi? Sasa rudi nyuma. Hii ni upande huu wa Biblia. Lazima upate historia. Wakatoliki

wanaamini katika miungu wengi, na walivunja Mungu mmoja wa kweli kuwa miungu watatu mbalimbali.

90 Na unisikie. Ni jambo baya jinsi gani lililokuwa kwenye gazeti hivi majuzi, kuhusu mtu mashuhuri ambaye sote tunamjua kuwa mtumishi wa Mungu; Billy Graham. Tunalo hilo tamshi. Ndugu Beeler, pale, analo. Alipoulizwa, Billy Graham, na *fulani*, "Nani, huu utata mkuu kuhusu utatu ulikuwa ni nini? Je, kulikuwa na miungu watatu, miungu watatu halisi? Au, ilikuwaje? Mahali pamoja, ilionekana kama miungu watatu. Na pengine ikaonekana kama kuna mmo-. . . " Billy Graham akasema, "Haijafunuliwa. Hakuna anayejua." Jamani!

91 Ikiwa kuna miungu watatu, sisi ni makafiri. Kama yule Myahudi alivyosema, "Ni yupi kati yao aliye mungu wenu? Baba? Je, Mwana ndiye Mungu wenu? Au, Roho Mtakatifu ndiye Mungu wenu?" Mungu ni mmoja tu.

Na hao si watu watatu, kwa maana utu hauna budi kuwa mtu. Haiwezi kuwa utu bila kuwa mtu. Mnajua hilo. Je, kitu chochote kinawezaje kuwa utu bila kuwa mtu?

92 "Loo," kasema, "hatuamini miungu watatu wa kibinafsi. Tunaamini katika nafsi tatu za Mungu mmoja." Naam, kabla ya kuwa utu, inabidi awe mtu.

93 "Ni nini basi?" ungesema. Sio miungu watatu. Ni ofisi tatu za Mungu yeye yule.

Yeye alikuwa ni Baba, hapo mwanzo, aliyening'inia juu ya ja—jangwa katika—katika mwali wa Moto, kijiti kilichowaka moto. Ubaba, Mungu, kama tu nilivyomalizia kusema, akijishusha, akishuka. Hicho kilikuwa ndicho kiwango cha juu zaidi. Roho, a—a—*agapao*, *Zoe*, U—Uhai wa Mungu Mwenyewe uliofanywa kwa mfano wa nguzo ya Moto. Na Yeye yule, baada ya kuwa katika Ubaba, akawa Mwana, na Roho wa. . .alikuwa kwenye kichaka kilichowaka moto, alikuwa katika Mwanadamu, Kristo, nayo ikaleta ushahidi ule ule ambao ule Moto ulileta. Kasema, "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi." Kila mti utatoa ushahidi wa tunda lake.

94 Na kisha baada ya kuwa Mwanadamu, mnaona, ilishuka kutoka kwenye mambo ya Kimbinguni, ikawa kitu dhahiri kinachoweza kuguswa, mwili. Na kupitia kifo cha dhabihu na dhabihu iliyo kuu sana ya huyu Mungu mmoja, Yesu, alisema, "Mimi na Baba Yangu tu Mmoja. Baba Yangu anakaa ndani Yangu." Unaweza. . .Hakuna mtu angeweza kusoma jambo hilo kwa uwazi zaidi.

Walisema, "Kwa nini usituonyeshe Baba, na ita—itatutosha." Yohana 14:8.

95 Akasema, “Nimekuwa nanyi kwa muda mrefu sana, na hamnijui Mimi?” Akasema, “Mnapoona Ba-. . .Mnaponiona Mimi, mnamwona Baba Yangu.”

Kama vile mwanamke mmoja alivyoruka juu wakati mmoja; akasema, “Mbona, Ndugu Branham,” akasema, “naam, Baba na Mwana ni mmoja, kama vile tu wewe na mke wako mlivyo mmoja.”

Nikasema, “Loo, hapana, sivyo.” Nikasema, “Unaniona mimi?”

Akasema, “Ndiyo.”

Nikasema, “Unamwona mke wangu?”

Kasema, “La.”

96 Nikasema, “Basi wao si aina iyo hiyo ya moja. Yesu alisema, ‘Mnaponiona Mimi, mmemwona Baba. Baba anakaa ndani Yangu.’ Mke wangu hakai ndani yangu.” Mnaona?

Wao ni Mmoja. Kwa kila njia, wao ni Mmoja. Nasi ni mmoja kwa makubaliano, mimi na mke wangu. Sisi ni wamoja katika ushirika, lakini sisi ni watu wawili. Mke wangu anaweza kufanya aina moja ya kuwazia, na mimi nyingine. Na sisi ni watu wawili. Lakini sivyo kwa Mungu. Wao, Mungu na Kristo, ni Mtu yule yule.

97 Basi Roho Mtakatifu ni nini? Roho Mtakatifu ni Roho yule yule wa Mungu akikaa ndani ya watu aliowafia, na kuweka jina lao kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Ambapo, walikuwa mmoja Naye, hapo mwanzo. Maandiko yanasema hivyo. Hivi Yesu hakuwaambia kwamba walikuwa pamoja Naye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? Akili zenu zimetiwa giza na ni nyeusi, na sisi sote tuko hivyo, kwa mambo hayo. Lakini sisi sio bahati tu ndogo inayotokea hapa. Sisi ni wana na binti za Mungu, katika mwanzo wa uumbaji wa Mungu, nasi tumeshushwa hapa chini kwa ushuhuda, kushuhudia neema ya Mungu iliyomiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu. Tuna Roho wa Milele. Hakuna mtu, hakuna mtu, na hakuna njia, ya kumzuia. Kanisa la Mungu litakuwepo kwa uhakika tu kabisa.

98 Tulipokuwa tunazungumza, kuchukua somo hilo dogo tena, kwa—kwa dakika moja, jinsi mtoto wa haramu asingeweza kuingia katika ufalme kwa vizazi kumi na vinne, miaka mia nne, na jinsi uovu wa wazazi ulivyowapata watoto, hata kizazi cha tatu na cha nne.

99 Pia, haki ya wazazi ilipatilizwa. Unachofanya, ikiwa kuna kesho inayokuja na una kitukuu, tendo lako leo litaamua atakuwaje basi.

Kwa maana tunasoma katika Biblia ambapo huyo Melkizedeki, alipokutana na Ibrahimu akirudi kutoka katika kuwapiga wafalme, naye Ibrahimu mzee wetu akampa sehemu

ya kumi ya yote aliyokuwa nayo. Na kisha akasema hivyo juu ya zaka, kwamba, "Lawi pekee ndiye angeweza kukubali zaka. Lakini," akasema, "Lawi, ambaye alitwaa sehemu ya kumi, alitoa zaka alipokuwa bado katika viuno vya Ibrahimu."

100 Loo, unaweza kushika hilo? Ibrahimu alikuwa nanii wa Lawi. . .kitukuu. Na hapa, Lawi, angalau miaka mia nane au elfu moja baadaye, labda mia kadhaa. Nisingejua ni mingapi hasa, mingi. Ingebidi kuihesabu, kupitia kizazi. Lakini, Ibrahimu alimzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo; Yakobo akamzaa Lawi. Na hapa, Lawi, Yakobo angekuwa baba yake; Isaka babu yake; na Ibrahimu babu wa baba yake. Na wakati Yakobo alipokuwa katika viuno vya Ibrahimu, Biblia ilisema, "Alitoa zaka kwa Melkizedeki."

101 Na kisha kizazi hiki cha vijana, wakikimbia huku na huko, wakivuta sigara, wakinywa pombe, na kila kitu, mnatarajia kizazi kingine kiweje? Sababu ya sisi kuwa na dhambi, uasi wa watoto sasa, sababu ya sisi kuwa na wasichana wadogo mitaani, na wavulana wadogo, ni kwa sababu mama na baba zao walifanya walichofanya katika wakati wao uliopita.

Na sababu ya sisi kuwa tungali tuna wahubiri ambao wataitetea Kweli, sababu ya sisi kuwa bado tuna wasichana wa mtindo wa kale, ni kwa sababu walikuwa na wazazi wa mtindo wa kale. Hiyo ni kweli kabisa. Bado tuna wahubiri ambao husimama bila kupatana na madhehebu yoyote, ama Neno, ni kwa sababu tulikuwa na wahubiri wa mtindo wa kale huko nyuma, waliosimama moja kwa moja kwenye misingi ile ile. Naam.

102 Sasa tuko katika siku hii. Na sasa tunataka kusema, ya kwamba, humu ndani, tukirudi kwenye. . .baadhi ya madhehebu, sababu ya sisi kuwa si dhehebu. Na, kwa sababu, kama tungekuwa dhehebu, ingetubidi kulisujudia hilo.

103 Pia kumbukeni, chunguza Maandiko popote unapotaka, nawe hutapata mahali hata pamoja katika Biblia ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa kwa kunyunyiziwa, kwa kumwagiliwa, au kwa jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Kwa hiyo, kama hauko katika Maandiko, ilibidi uanzie mahali fulani.

104 Kama ninavyosema, nimeketi chini ya mti mkubwa, nikiutazama. Huo, loo, huenda ukawa kama wa—wa kiume, hu—huenda ukawa mkubwa mno, huenda ukawa na nguvu, lakini ulikuwa na mwanzo. Ilibidi uanze. Na kila kitu. . . Dini hii ya zamani ambayo tunaisimamia kwa ushujaa sana, ilibidi ianzie mahali fulani. Ilibidi iwe na mwanzo. Nazo itikadi tulizo nazo, ilibidi ziwe na mwanzo. Na Maandiko ya uwongo tunayotumia katika madhehebu yetu, ilibidi yawe na mwanzo. Na kama tukisema, "Mimi ni Mmethodisti," ilibidi uwe na mwanzo. Ukisema, "Mimi ni Mbaptisti," ilibidi uwe

na mwanzo. Unasema, “Mimi ni Mkatoliki,” ilibidi uwe na mwanzo. Unasema, “Mimi ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili,” ilibidi uwe na mwanzo. Ilibidi uwe nao.

105 Rudi nyuma, uone mahali ulipoanzia. Wacha turudi kwenye mwanzo wa picha. Basi kama hakuna dhehebu katika Biblia, basi dhehebu ilibidi liwe na mwanzo. Lilianza na kanisa Katoliki. Waprotestanti walitokana tu nalo.

106 Basi kama Biblia ilisema ya kwamba alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya, kwa sababu, fundisho lake, alifanya uasherati wa kiroho. Uasherati ni nini? Kumbuka, tuliupitia sasa. Mwanamke anayeishi na mumewe, yeye ni sawa na bikira. Hajawahi kutiwa najisi, maadamu anaishi na mwanamume huyo mmoja. Lakini udhalimu ni nini? Haki, iliyopotoshwa. Mwache aishi na mwanamume mwingine, naye amehukumiwa. Mnaona? Haki, iliyopotoshwa.

107 Sasa, kama dhehebu lilikuwa ni makosa . . . Kama lingekuwa sahihi, Mungu angalisema, “Sasa tutakuwa na madhehebu.” Na kama . . . Kanisa Katoliki lilitajwa, katika Biblia, kama “kahaba,” dhalimu, kwa sababu lilikuwa likilipa kusanyiko lake theolojia yake mwenyewe, wala si Biblia. Ndugu, dada, je, kanisa Katoliki haliwacheki hadharani kuhusu Biblia? Wanasema hawajali Biblia inasema nini; ni yale kanisa lisemayo, yale dhehebu lao lisemayo. Vema, basi, unawezaje kusema wamekosea wakati utaukimbilia ubatizo wa “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” wakati Biblia inauhukumu? Ati kwa sababu Wamethodisti wanasema hivyo, Wabaptisti wanasema hivyo? Kwa nini utakubaliana na kunyunyizia na kumwagilia, wakati hakuna kitu kama hicho kwenye Biblia? Hakuna kitu kama mtu yeyote kubatizwa kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Basi kwa nini unafanya hivyo?

108 Unaona, hiyo ndiyo sababu sisi si dhehebu. Haitulazimu kuwashughulikia. Tunachukua . . . Wakati Roho anapotupa Nuru kwenye Maandiko, tunadumu na Maandiko na BWANA ASEMA HIVI. Haya basi. Hakuna vitu kama hivyo. Haijaandikwa katika Maandiko.

109 Loo, unasema, “Vipi kuhusu Mathayo 28:19?”

Sasa, tumepitia hilo mara kadhaa. Hiyo ilikuwa ni hoja ambayo Yesu alisema. “Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Je, iliwahi kutekelezwa? Je, kuliwahi kuwa na mtu aliyewahi kubatizwa kwa njia hiyo? Si hata mmoja. Basi lazima kuna kasoro mahali fulani. Hakika, ni Ukatoliki uliofanya hivyo.

110 Tafuta kujua kama kuliwahi kutokea katika historia, hadi wale waanzilishi waliotangulia Nikea, ninyi wanahistoria. Someni vitabu vya wale waanzilishi waliotangulia Nikea, muone, hata kufikia kwa mfalme wa Uingereza. Kila mmoja

wao alibatiza katika Jina la Yesu Kristo mpaka kanisa Katoliki. Na kanisa Katoliki lina nguvu, walisema, kubadilisha chochote watakacho. Nao wakaanza kubatiza kwa jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Martin Luther aliutoa. John Wesley akaufuatilia. Naye Alexander Campbell akaja na huo. Ndipo John Smith, wa kanisa la Baptisti, akafuata. Hii hapa Pentekoste ikiendelea nao, bado.

Lakini saa imewadia!

111 Tazama vinara vya taa, kama tulivyokuwa navyo jana usiku. Kinara cha kwanza cha taa ni Nuru. Ilizidi kuwa giza zaidi, zaidi, zaidi, mpaka ikapitia kwenye ile miaka elfu moja na mia tano ya nyakati za giza. Kisha, ikaanza kumulika. Na kabla tu ya wakati wa mwisho wa kanisa, ikamulika tena. Katikati ya hizo nyakati mbili za kanisa, Nuru ikaja.

Fuata Maandiko, ya kanisa la Efeso, kanisa la Thesalonike, na kuendelea hadi kwenye wakati wa giza. Kila mmoja wao, Yeye alisema, "Una nguvu kidogo, lakini hujalikana Jina Langu." Na kanisa linalofuata, "Umefanya jambo kubwa, lakini hujalikana Jina Langu." Wafuatilie waanzilishi waliotangulia Nikea kupitia hiyo. "Wewe hujalikana Jina Langu." Kisha, miaka elfu moja na mia tano ya nyakati za giza.

Ndipo kanisa la Kilutheri likatoka. Yeye akasema, "Hamna Jina Langu, lakini mnalo jina." Si Yesu tena; bali Luther, na Katoliki, na Baptisti, na Presbiteri. "Mna jina kuwa mu hai. 'Sisi ni kanisa hai. Tunastawi. Tunaendelea.' Lakini mumekufa!" Maandiko yalisema hivyo.

112 "Kwa maana hapana jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu ambalo wanadamu wanaweza kuokolewa kwalo." Sivyo. . .Baptisti haikuokoi. Presbiteri haikuokoi. Katoliki haikuokoi. Yesu anakuokoa.

113 Wote katika vitabu vidogo vya kiada, nadharia za kujibunia, waliziweka chini, "Hilo ndilo tunaloamini." Na hiyo ndiyo sababu tunakaa mbali nayo. Hatuna kitabu cha kiada ila Biblia. Hakuna uongozi, hakuna askofu, ila Roho. Hiyo ni kweli.

Na basi kama kuna roho mbaya anayeingia, atakayejaribu kugeuza kitu fulani mle ndani, Neno litakirekebisha. "Hayo ni makosa. Kaa mbali nayo." Unaona? Huyu hapa Roho anakuja, akisema, "Hayo ni makosa." Anashuhudia, kwani roho zetu hushuhudia pamoja na Roho Wake.

Hapa anakuja mmoja, akisema, "Loo, tunapaswa. Loo, nafikiri ni sawa kwao kufanya *hili*, *lile*, *linginelo*."

114 Lakini Roho akasema, "Kuna kasoro hapo." Inarudi moja kwa moja katika Biblia na kumshusha moja kwa moja, jinsi tufanyavyo. "Na ni makosa. Kaa mbali nayo."

Hiyo ndiyo sababu Biblia ilisema, "Hii hapa kwake yeye aliye na hekima. Hii hapa kwa mwenye ujuzi. Hii hapa kwake

yeye aliye na *hii*." Kanisa pale, limekaa katika utaratibu. Hivi hamwoni ule mpango mkuu wa Mungu?

115 Sasa tazama. Wakati wa Kanisa la Filadelfia ulikuwa ndio wakati wa kanisa la Methodisti, wakati wa kanisa wa upendano wa kidugu, yale matengenezo. Ambayo, wakati kundi la Ukalvinisti lilikuwa limeinuka katika kanisa la Anglikana huko Uingereza, ambako hata hawakuwa na uamsho tena, waliingia hadi kwenye mbegu za nyasi kavu, Mungu alimwinua John Wesley kama mshika sheria, kuchukua fundisho la Kiarminia. Ndipo alipofanya hivyo, alikigonga kitu hicho kichwani, na kilistahili kugongwa. Lakini alifanya nini? Hawa hapa Wamethodisti wakaja, na kukimbia upande *ule* kama vile yeye (Wakalvini) walivyokimbia upande *huu*. Sasa, hapo katikati, angali Mmethodisti, angali Mbaptisti.

116 Laiti tungeweza kufika hapa sasa katika Maandiko, tuchukue Ufunuo 3, nanyi mtalipata. Sasa kabla tu. . . Wakati wa mwisho wa kanisa, ambao ulikuwa wa Kipentekoste, ni Wakati wa Kanisa la Laodikia, wenye uvuguvugu, ambao umekataliwa.

Lakini kumbukeni, kama Yesu alivyoonekana msalabani, amesimama katika vile vinara vya taa saba vya dhahabu, uliokuwa na giza zaidi ni ule uliokuwa mbali zaidi Naye, mkono Wake wa kulia na mkono Wake wa kushoto. "Naye alionekana mithili ya Alfa na Omega." Sio wa katikati. "A—Alfa na Omega," kama alivyonyoosha mkono Wake. "Naye alikuwa jiwe la yaspi na akiki," ambayo yalikuwa ni Benyamini na Rubeni, "wa kwanza na wa mwisho." Huyo hapo ameinyosha mikono Yake. Huyo hapo amesimama.

117 Lakini kumbuka, wakati wa kutoka kwa hili, usilichanganye. Kwa maana, walipopokea majina haya hapa, ya madhehebu haya, wangekufa moja kwa moja katika mambo yale yale, moja kwa moja kuendelea. Lakini Yeye alisema, kati tu ya Wamethodisti na Wapentekoste, wakitoka, "Nimeweka mlango ulio wazi mbele yako." Haya basi, lile Jina kurejeshwa tena. "Nimeweka mlango ulio wazi. Kwa maana Mimi ndimi Njia, Kweli, na Uzima. Mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya Mimi." Ni nini? Mlango wazi huo.

118 "Mlango-bahari!" Mlango-bahari, ikiwa uliona, sio s-t-r-a-i-g-h-t. Ni s-t-r-a-i-t. [Kiswahili: M-n-y-o-f-u. M-l-a-n-g-o-b-a-h-a-r-i—Mfas.] "Mlango-bahari ndiyo njia." Mlango-bahari, ni maji.

Vipi? "Rudini kwenye Jina la Yesu, ambalo mlikuwa nalo. Hamna. . . Mna maisha kidogo; hamjalikana Jina Langu." Ndipo, basi, *hapa* ndani walilipoteza, wakaingia katika dhehebu la Katoliki; wakatokea katika dhehebu la Kilutheri, wakatokea katika dhehebu la Wesley, ndipo wakaingia moja kwa moja kwenye Upentekoste basi.

Lakini, kabla tu ya wakati wa mwisho, ule Uzao uko karibu kuondoka duniani. Umefifia, Uzao wa wenye haki. Uzao wa nyoka unaongezeka haraka zaidi na zaidi na zaidi, ukijitayarisha kwa ajili ya wakati huu wa atomiki, kuangamizwa. "Lakini kabla tu ya wakati huo, nitaweka njia ya kuepukia. Nitaweka mbele yako mlango wazi. Mlango huu ni mwembamba na njia hii imesonga, na kutakuwa na wachache tu wao ambao wataipata. Lakini njia ni pana iendayo upotevuni, na wengi watapitia humo." Haya basi. Kabla tu ya jambo hili, Nuru hii kuu ilipaswa kutokeza.

119 Nimefurahi sana. Sijui kamwe jinsi ya kulielezea, nina furaha sana. Huu hapa, wakati wa kufunga, na sijagusa somo langu.

120 Ninataka kuzungumza juu ya: *Ubatizo wa Roho Mtakatifu*. Nitaligusia, kwa vyovyote vile, kwa dakika kumi, kumi na tano. Sasa, sitawaweka saa tatu kama nilivyofanya jana usiku; nitajaribu kutowaweka.

121 Sasa, kama wana ubatizo wa uwongo wa maji, madhehebu yamekosea. Na yeyote anayetetea dhehebu fulani anaunga mkono kabisa jambo lisilofaa. Wanaunga mkono kile ambacho Mungu anapinga. Alisema hivyo katika nyakati hizi za kanisa. Alisema hivyo katika Maandiko, na kuwaita makahaba, kwa sababu, "Wanafundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." Sasa, sisi . . .

122 Nilienda mahali fulani si muda mrefu uliopita, kwa mtu fulani aliyekuja hapa, akiandika tasnifu juu ya uponyaji wa Kiungu. Naye akasema, "Jambo pekee kukuhusu wewe, Ndugu Branham," kasema, "watu wanakukosoa kwa sababu unawaendea Wapentekoste."

Nikasema, "Kweli, nitakuja kwa yenu," nikasema, "kama mtaniunga mkono katika mji wenu."

Akasema, "Vema," kasema, "tayari ni—ninalifuatilia hilo." Kasema, "Nililipeleka kwa askofu wa kanisa hili *fulani*, kanisa la Methodisti." Hakuna haja ya kulichezea. Akasema, "Nililiwasilisha, nao wakasema, 'Sasa, unaona, sisi, kama kanisa la Methodisti, hatuamini katika miujiza hii.'"

123 Sasa utafanya nini? Sasa utasikiliza kanisa la Methodisti, ama hilo dhehebu? Ikiwa utayasikiliza, wewe ni kahaba wa kidini. Unafikiri kanisa la Baptisti lingeunga mkono uamsho kama huo? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Kwa nini? Kwa sababu wao ni Wabaptisti. Biblia ilisema wao ni makahaba. Alizaa binti zake, nao walikuwa ni "makahaba." Kwa nini? Wakitoa aina ile ile ya fundisho, fundisho la kujibunia, badala ya Fundisho la Mungu. Hiyo ndiyo sababu hatujajifanya dhehebu pamoja na Wabaptisti. Hiyo ndiyo sababu hatujajifanya dhehebu pamoja na Wamethodisti.

124 Sasa, kwa nini sisi hatujajifanya dhehebu pamoja na Wapentekoste? Haya basi. Hivyo ndivyo hasa. Mpentekoste angekaa ambapo. . . Kama—kama kanisa la Kilutheri lingekaa pale ambapo lingeanzia, lingekuwa la Kipentekoste. Lakini walifanya madhehebu, kwa hiyo Mungu akamwinua mpentekoste mwingine, anayeitwa Wesley. Na kwa hiyo wakati Wesley alipounda dhehebu, Yeye aliinua jingine, lililoitwa Baptisti. Walipojiundia dhehebu, basi Yeye akaliinua jingine, lililoitwa Wakampbeli. Walipounda dhehebu, Yeye akainua jingine, liloloitwa Pentekoste. Wanapounda dhehebu, Yeye anasonga mbele. Angalia tu uone.

125 Sio mpango wa Kiungu wa Mungu. Haliko katika mpango wa Mungu, kuwa na hayo madhehebu. Kwa hiyo, unaona, hiyo ndiyo sababu sisi si dhehebu.

126 Kumbuka hili. Nilisema, hapo mwanzo, sasa, ikiwa nitakuudhi, sikusudii. Hili ni kwa ajili ya kanisa. Kama unaketi nasi, tunapenda kuwa nanyi hapa, lakini hili ndilo tunalotetea, na ndiyo sababu sisi si dhehebu.

127 Sasa, dhehebu, kwanza kabisa, ni la uwongo, na ni waalimu wa uwongo. Nilisema litaumiza, nami nataka liumize. Ni walimu wa uwongo kabisa. Mtu yeyote anayejua mambo hayo, na atasimama na kupatana, kwa ajili ya Mbaptisti, Mmethodisti, Mlutheri, au Mpentekoste, akijua ya kwamba Biblia inafundisha tofauti, yeye ni nabii wa uwongo. Hakuna kubaki humo. Hiyo ni kweli hasa. Hiyo ndiyo sababu sikujiunga na Assemblies. Hiyo ndiyo sababu sikujiunga na Umoja. Hiyo ndiyo sababu sikujiunga na Baptisti, Methodisti, au Mpresbiteri, kwa sababu wao ni waongo. Simaanishi watu wao ni waongo. Ninamaanisha theolojia yao ni ya uwongo, kwa sababu hailingani na Neno la Mungu.

Paulo alisema, "Kama. . . " Alikwenda hapa. . . Hebu niwaonyeshe kile Paulo alichosema, kabla hatujaacha ubatizo huu wa maji.

128 Yesu alipotoa hiyo hoja, katika Mathayo 28:19; Petro, siku kumi baadaye, alisema, "Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

Wakati mwingine ubatizo ulipotajwa, ni wakati mwinjilisti Filipo aliposhuka na kuwahubiria Wasamaria. Naye akawabatiza kila mmoja wao katika Jina la Yesu Kristo. Paulo. . . Petro alishuka, ama Petro na Yohana, hasa, na kuweka mikono juu yao; wakampokea Roho Mtakatifu.

Kisha wakapanda kule juu. Petro akaenda moja kwa moja basi hadi nyumbani kwa Kornelio. Na wakati Kornelio. . . "Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia." Petro akasema, "Hatuwezi kuzuia maji, kwa kuwa hawa wamempokea Roho Mtakatifu sawa sawa na sisi

hapo mwanzo." Naye akaamuru wabatizwe katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

129 Sasa, Paulo akapitia pwani ya juu ya Efeso; akawakuta baadhi ya Wabaptisti. Nao walikuwa na—wao wana mtume kule juu, mtume wa Biblia, na jina lake lilikuwa Apolo. Alikuwa mwanasheria, aliyeongoka, naye alikuwa akiwathibitishia hao watu ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo, kwa Biblia. Akasema, "Ma—Masihi anapaswa kufanya mambo fulani. Mtu huyu alikuwa ndiye Masihi."

130 Nao walikuwa na kundi kubwa la watu pale, nao walikuwa wakishangilia, na kupiga makelele, na kuwa na wakati mzuri sana. Akila na Prisila walikuwa wameenda kule na kuungana nao, wakiwa na ushirika pamoja nao. Hawakuwa na dhehebu. Walikuwa na ushirika. Na kwa hiyo wakaona mtu huyu alikuwa mtu mashuhuri, loo, yeye ni mwerevu, wakili, naye alikuwa—alikuwa mtu mwerevu. Hivyo yeye . . . Wakasema, "Sasa, wewe, wewe ni mzuri sana kwa kile unachojua, lakini tunaye maskini ndugu mmoja jina lake Paulo. Atakapokuja, amekuwa na ujuzi fulani, anajua anachozungumzia. Atawafundisha njia ya Bwana kwa uwazi zaidi, kama mtatulia tu na kumsikiliza. Sasa, msijaribu kumsukumia jambo fulani, maana hatalivumilia. Mnaona? Lakini ninyi—ninyi endeleeni tu, msikilizeni."

131 Ndipo Paulo akapitia kule. Akawasikiliza, akitazama huko mara moja.

Akasema, "Hilo ni zuri sana, lakini je, mmempokea Roho Mtakatifu, ninyi Wabaptisti, tangu mlipoamini?"

"Loo," wakasema, "hivi hatujampokea?"

"Sidhani." Unaona?

"Vema, kwa nini?"

"Naam, mlibatizwaje?"

"Loo, tumebatizwa. Tumebatizwa."

132 "Vema, ni nani aliyewabatiza? Na mlibatizwaje?"

Biblia inasema, "jinsi gani." Kigiriki, au ya asili, inasema, "kwa njia gani." Na hii inasema, "*mlibatizwaje*." Kasema, "Mlibatizwa namna gani?" Kwa maneno mengine, "Mlibatizwaje?"

133 "Tulibatizwa na Yohana Mbatizaji, mtu yule yule aliyembatiza Yesu Kristo, shimo lile lile la maji."

Huo ni ubatizo mzuri sana, hamdhanii hivyo? Inaonekana kana kwamba huo ungetosha kabisa, sivyo? Inaonekana kama ungekuwa sawa, kama ni yule mtu aliyeingia majini pamoja na Bwana wetu Yesu Kristo na kumbatiza Yesu. Naye Mungu akauidhinisha, mpaka akashuka katika umbo la Roho Mtakatifu na kuingia ndani Yake. Naye akasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani yake," mara tu baada

ya ubatizo huo. Inaonekana kwangu kama ubatizo huo ulikuwa sawa.

134 Naye Paulo akasema, "Hautafaa tena sasa. Hautafaa tena."

"Kwa nini hautafaa tena?" Mnaona?

"Hamna budi kubatizwa tena."

"Unamaanisha kwamba sisi, tuliobatizwa na Yohana, aliyembatiza Yesu, inabidi tubatizwe tena?"

"Hiyo ni kweli."

Kasema, "Tunapaswa kubatizwa kwa njia gani?"

135 Kasema, "Katika Jina la Yesu Kristo."

Ndipo Paulo akawapeleka huko nje na kuwabatiza wote, tena. Matendo 19:5. "Ndipo waliposikia hili, walibatizwa tena, sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Naye Paulo akaweka mikono yake juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu."

136 Kama Paulo aliwashurutisha wanaume na wanawake kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo; kama nikihubiri injili nyingine yoyote, basi roho yangu haiko sawa kama ya Paulo ilivyokuwa. "Na atambue yale ninayoandika ni maagizo ya Bwana."

137 Na sasa katika Wagalatia 1:8, Paulo alisema, "Kama malaika kutoka Mbinguni akija, malaika mwenye kung'aa sana." Anazungumza juu ya nini? Ufunuo. Jina la Bwana libarikiwe! Haijalishi jinsi ufunuo wako ulivyo mzuri. Mnakumbuka ibada yetu ya kwanza asubuhi ya leo, Urimu Thumimu? Kama kitu kikija na kulifunua kikamilifu; yeye ni mwongo, yeye ni malaika wa uwongo, naye mtu anayebeba ujumbe wake ni nabii wa uwongo. Kuna njia moja tu ya kubatizwa, hiyo ni Jina la Yesu Kristo. Ikiwa hujabatizwa hivyo, kuna mahali pa kubatizia panapongojea. Hiyo ni kweli.

138 Si kweli! Nitafutie mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Haiko katika Maandiko matakatifu. Ni nini? Ni fundisho la sharti lililoanza na kanisa Katoliki. Tunaweza kuunga mkono hili. Tunayo mafundisho kamili ya wale waanzilishi wa Nikea. Tuna historia yake. Tunacho *Babeli Mbili* cha Hislop. Tuna maandishi ya Josephus. Tunazo historia zote za kale. Naye Josephus aliandika katika wakati wa Bwana Yesu. *Babeli Mbili* cha Hislop, kilichoandikwa baada ya hapo. *Waanzilishi Waliotangulia Nikea* kilichoandikwa baada ya hapo, kabla ya kuanzishwa kwa kanisa Katoliki. Kisha kanisa Katoliki likaingia, na kuwasukuma wote na kutwaa mamlaka, wao wenyewe, ndipo Rumi ya kipagani ikafanywa Rumi ya kipapa. Na hapo wakaleta huo ubatizo wa uwongo wa maji, kwenye kunyunyiziwa; na kutoka katika Jina la Bwana Yesu, hadi "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Naye Yesu akasema, chini ya uvuvio aliompa Yohana pale Patimo, "Una jina la kuwa

hai, lakini umekufa." "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni jina la kufa.

139 Hebu niwaambie ujuzi mdogo wa kibinafsi; Uswisi, Ujerumani, na maeneo ambayo nimekuwa.

Wapiga ramli hufanyaje kazi? Pepo wachafu husafiri vipi? Ninawatakeni mniamini, kama mchungaji wenu, maana ninyi ndio ninaozungumzia. Mashetani husafiri kwa jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Wanakata manyoya, na chochote kile, na kunuiziana uchawi, kupitia jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," wanayaita majina matatu makuu. Mama yake ni makanisa ya Katoliki. Wanaziendea sanamu hizi ndogo na kupiga magoti pale, na kukata unyoya kwa makasi, na kuurudisha nyuma, na kuwanuizia uchawi majirani zao, na kadhalika, ambapo wanachomwa moto hadi kufa, na chochote kile, kwa ajili yake.

140 Huko Uswisi, nimesimama nimeweka mikono yangu juu ya nguzo, namna *hiyo*, ambapo wanaume na wanawake waaminifu walikufa, walipokata ndimi zao, na kuyachoma macho yao, na kila kitu, kwa fito za chuma cha moto, lile kanisa kahaba la Katoliki. Isitoshe, bali makanisa yenu ya awali ya Kianglikana, pia. Na makanisa yenu ya Kiprotestanti yalifanya jambo lile lile. Nao walinuiza uchawi huo, kwa "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu."

141 Ndugu yenu na mchungaji wenu, nimekuwa na—na fursa ya kushukuru, kwa neema ya Mungu, kulindwa katika mambo haya, lakini kujua yakini nilichokuwa nikizungumzia. Ambapo, mwanamke, alikuja kwenye kanisa hili, akanihukumu na kusema, "Anajipumbaza na mizimu." Mungu aliye Mbinguni anajua yote yalivyokuwa. Siwezi kuchukua mtu yeyote . . . sikuninii . . .

142 Waliponiambia kwamba Pigalle, huko Paris, palikuwa mahali penye sifa mbaya sana, nilijuaje? Sikuwahi kuwa huko. Lakini nilishuka kwenda kule ili kujua kama ilikuwa ni kweli au la. Nikachukua wahudumu wengine wawili au watatu kisha nikashuka kwenda kule kwa hao wanawake na kadhalika waliovua nguo kwenye barabara hizo na kadhalika. Ni ukweli.

143 Nilijuaje Rumi ilikaa juu ya vilima saba? Nilijuaje kuwa papa alikuwa na VICARIVS FILII DEI? Ilibidi kuamini neno la mtu mwingine kwa ajili yake. Nilijuaje taji yenye sehemu tatu ilikuwa juu ya papa; utawala wa kasisi wa Mbingu na nchi na kuzimu? Nilijuaje mpaka nilipoenda na kuiona?

144 Nilijuaje kuna Mungu aliye hai? Sio chini ya theolojia ya mtu fulani, dhana fulani ya kiakili ya kipindi fulani cha mihemko kilichopitia kwenye wakati uliopita, kama vile makafiri wangetwambia. Lakini siku moja, kule chini, nilikutana Naye na kuzungumza Naye, uso kwa uso. Hilo lilifanya mambo kuwa tofauti. Kweli kabisa.

145 Mizimu hufanya kazi kupitia "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Nilisimama kwenye mkutano ambapo wale wachawi walikuwa wanafanya kazi. Usifikiri hawatakupa changamoto. Walisimama pale. Wakarusha meza juu hewani, nayo ikaelea kote; huku gita inacheza. Wakiwa wamesimama pale, nao walikuwa wanataka kunyamazisha. Nikasema, "Mmekosea." Nayo roho ikanena nao, roho iliyodai kuwa ni Mungu, ikasema ni Mungu. Nikasema, "Ni uwongo. Ni ibilisi."

Wakasema, "Mtu huyu ni kafiri."

146 Nikasema, "Mimi siamini upuuzi huu, kwa sababu si ya Bwana wangu. Huu ni uchawi. Huu ni wa ibilisi." Nikasema, "Sasa, hapa nitajaribu Jina hilo lenye nguvu nililobatiziwa." Nikasema, "Kwa jina la 'Mbingu za juu,' niambie ukweli." Hata hakunijibu. Nikasema, "Kwa jina la 'Kanisa takatifu,' niambie ukweli." Hakunijibu. Nikasema, "Kwa jina la 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,' niambie ukweli." Naye hakunijibu. Lakini, nikasema, "Kwa jina la 'Yesu Kristo,' niambie ukweli."

147 Akasema, "Ndiyo. Si kweli." Mungu anajua hiyo ni kweli. Naam, bwana.

> Loo, imani katika Baba, imani katika Mwana,
> Imani katika Roho Mtakatifu, hawa watatu ni Mmoja;
> Pepo watatetemeka, wenye dhambi wataamka;
> Imani katika Bwana Yesu hufanya kitu chochote kutikisika.

Naam, bwana. Dumu na Jina hilo.

148 "Una jina la kuwa hai, lakini umekufa." Hilo hapo kanisa lako. Hilo hapo.

149 Sikilizeni. Kuna mwanamke mmoja ameketi. . .Kuna wanawake wazuri, wenye sura nzuri, warembo wanaoketi katika kanisa hili asubuhi ya leo. Wasichana, wanawake wa makamo, wanawake wakongwe, wote wako sawa. Wao ni mke wa mtu fulani, binti ya mtu fulani, mchumba wa mtu fulani, kadhalika. Wao, kila mmoja. Kuna Bibi Branham mmoja anayeketi hapa. Ninyi, kila mmoja, ni wanawake. Lakini kuna Bibi William Branham mmoja. Yeye ndiye anayeenda nami nyumbani. Yeye ndiye mpenzi wangu. Yeye ndiye anayelea watoto wangu.

150 Kuna makanisa mengi mazuri ulimwenguni leo. Lakini kuna Bibi Yesu mmoja ambaye anazaa viumbe halisi, wa kweli, wa Mungu, waliozaliwa mara ya pili. Mnajua ninachomaanisha, sivyo? Jina lake si Methodisti. Jina lake si Baptisti. Jina lake ni Yesu, Bibi Yesu. Hakika, ndivyo alivyo. Anawazaa watu, si washiriki wa kanisa la Methodisti. Yeye hazai kanisa la Kibaptisti, ama Presbiteri, au Katoliki. Anawaleta, waliozaliwa, na kuwa na shina na msingi katika Kristo Yesu. Huyo hapo. Huyo Ndiye. Nina furaha sana kuwa niko pamoja Naye. Yeye

ni Kanisa la kisiri. Yeye hana dhehebu lolote. Habebi lolote la majina haya makubwa ya kifahari na majengo makubwa. Yeye hukutana popote washiriki wa huo Mwili hukusanyika pamoja. Wanaabudu katika Roho na katika Kweli. Walichaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Andiko moja zaidi, nami ninawaahidi nitafunga. Nami nitaacha mengine hadi usiku wa leo. Leo, unaweza kukamata hilo usiku wa leo, basi.

151 Hebu twende kwa Waefeso, kwa dakika moja tu. Tusome tu Andiko hili moja, kisha nitawaachia hilo. Tunaona kile ambacho Biblia ilisema sasa kuhusu jambo hili. Nitamchukua mwalimu huyu mashuhuri, Paulo, ambaye ni. . .Hakujawahi kuwa na chochote kama yeye. Alikuwa mtume kwa Kanisa la Mataifa. Vema. Fungueni Waefeso 1.

152 Sasa tutafunga, katika dakika moja tu. Sikiliza hili, rafiki yangu mpendwa. Msikilize Paulo akilihubiria Kanisa la aina ile ile niliyo, asubuhi ya leo.

> *Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya. . .* (Kanisa la Presbiteri? Kanisa *gani*?) *. . .mapenzi ya Mungu kwa watakatifu* (waliotakaswa) *walioko Efeso,. . .*

Sasa, kumbukeni, wametawanyika kote ulimwenguni. Lakini, hili ni kundi lililoko Efeso, analozungumzia. Sasa, haongei na ulimwengu. Hazungumzi na washiriki wa kanisa la mahali hapo. Anaelekeza hili kwa waliotakaswa. Hebu tuone.

> *. . .na kwa wanaomwamini Kristo Yesu:*

Je, tunaingiaje ndani ya Kristo Yesu? "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa," kuishi kwa uaminifu. Unajuaje kuwa una Roho Mtakatifu? Tutashughulikia hilo labda usiku wa leo. Mnaona? Sawa.

> *. . .katika Kristo Yesu:*
>
> *Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na. . .Bwana Yesu Kristo.*
>
> *Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho. . .*

153 Unajua, haihitaji kupiga mayowe kwingi. Haihitaji mayowe mengi. Hiyo ni sawa; hakuna chochote dhidi yake. Ni sawa. Haihitaji hayo. Inahitaji mo—moyo uliojitolea, ukiketi katika ulimwengu wa Roho, ukila mambo ya Roho. Naye Roho hula nini, mhemko? Sio kwa jumla. Inaleta mhemko. Mnaona? Lakini ungeweza. . .

154 Kumbukeni. Mnakumbuka lile ono kuhusu mvua na ngano, yale magugu? Kumbukeni. Mvua inapohitajika, kuna gugu dogo, kichwa chake kimeinama chini; kichwa cha ngano kimeinama

chini. Mvua ikija, wote wawili wanaruka juu na kupaza sauti. Mvua ile ile. "Lakini kwa matunda yao mtawatambua." Angalieni.

*Neema na iwe kwenu,...zitokazo—zitokazo kwa Mungu baba yetu,...*

Sasa tazama. "Kama vile..." Kifungu cha 4 sasa.

*Kama vile alivyotuchagua katika yeye...*

Katika uamsho wa mwisho? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Ati? ["La."] Tunapokuwa washiriki wa Baptisti au Meth-...? La. "Amechagua," kabla hawajafanya mkutano. Naam.

*...kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,...*

Alituchagua papo hapo. La, hatukumchagua Yeye. Alituchagua sisi. Mnaona? Alituchagua wakati huo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

*...ili tuwe watakatifu...*

155 Tulikuwaje watakatifu? Si kupitia yale tuliyofanya, bali yale aliyotufanyia, maana hatuwezi kuwa. Unawezaje kumfanya nguruwe awe mwana-kondoo? Ndugu Roy, ulifuga nguruwe na wana-kondoo, wote wawili. Huwezi—huwezi—huwezi kuwachanganya. Nguruwe huninii tu...yeye huzunguka huko na kula kila aina ya takataka awezavyo. Ataenda kwenye lundo la samadi na kula akashiba. Vema, husikii vibaya kuhusu hilo. Unafikiri kwamba nguruwe huyo yuko sawa tu. Yeye ni nguruwe mzuri tu. Hivyo tu. Lakini huoni mwana-kondoo karibu na hapo. Asingeweza kumwalika kwa chakula cha jioni; asingekuja. Hapana. Kuna nini? Maana, yeye ni nguruwe. Hebu nenda ukamwambie amekosea. "Mungu asifiwe, mimi ni nguruwe. Wewe endelea na kwako. Wewe shuka huko, uwe mtakatifu anayejifingirisha ukitaka." Haya basi.

"Ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako," lilisema Neno.

156 Sasa, si kwa sababu niliacha kula samadi, kukanifanya kuwa tofauti na nguruwe, unaona, kukanifanya nisiwe nguruwe tena. Hivyo sivyo. Lakini wakati asili yangu ilipobadilika. "Loo, walinizungushia ua, nadhani. Wakanizuia. Sipaswi kufanya *hivi*"? Loo, hapana. Huzuii chochote kutoka kwa hii. Unazaliwa tu mara ya pili. Ni hayo tu. Umebadilishwa tu. Hiyo ni kweli.

157 Lakini kama ungeweza kuiondoa roho kutoka kwa huyo—kwa huyo mwana-kondoo na kuiweka ndani ya nguruwe; mwana-kondoo huyo angefanya jambo lile lile. Nguruwe angefanya jambo lile lile roho ya mwana-kondoo ndani yake ingefanya, na huyo mwana-kondoo angegeuka nyuma moja kwa moja na kufanya jambo lile lile alilofanya nguruwe.

Sasa mnaona, enyi nguruwe, mahali mlipo? Mnaona? Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli. Mnaona? Wewe endelea na kupenda

mambo ya ulimwengu, vaa kaptura na kufanya mambo haya yote. Endelea mbele, inaonyesha kile ulicho.

158 "Kwa matunda yao mtawatambua. Je, mtu huchuma tini katika miiba?" Mnaona? Hapana, hapana. Unachuma tini kutoka mitini. Unapata matofaa kutoka kwa mitofaa. Unapata miiba kwenye miti ya miiba. Hiyo ni kweli.

Sasa, sikilizeni kwa makini sana sasa.

> *Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa* na ninii yake, *na mapenzi yake mema—mapenzi yake,*
>
> akiisha kutuchagua tangu zamani, usifiwe *utukufu wa neema yake, ambayo* ametufanya tukubalike *katika huyo mpendwa.*

159 Nani aliyefanya hivyo? "Kwa sababu niliacha kunywa pombe? Kwa sababu niliacha kuvuta sigara?" La. Alifanya hivyo. Alinifanya, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, nikubalike katika uwepo wa neema Yake. Hakuna nilichofanya. Sijawahi kufanya lolote kuhusu hilo. Sikuwa na jambo moja la kufanya nayo.

Nilikuwa nguruwe, kwa kuanzia. Nilikuwa mwenye dhambi, nilizaliwa katika familia ya walevi, nikalelewa kwenye mwanga wa mbalamwezi tulivu, nikiwa nimeketi kwenye pipa la wiski, jambo la aibu. Hiyo ni sawa. Mwuza pombe haramu wa Kentucky, sikuwahi kuvaa jozi ya viatu hadi nilipokuwa mvulana mkubwa. Nywele zikining'inia shingoni mwangu, nikiwa nimeketi pale juu ya kipipa cha pombe haramu, wakitengeneza pombe haramu.

Hata hivyo, Roho Mtakatifu alinijia, nikiwa na umri wa miaka saba, akasema, "Usiguse hata tone lake. Na usijipumbaze na hao wasichana wadogo huko nje. Wala usivute sigara au kutafuna tumbaku." Loo, jamani! Ilikuwa ni nini? Mapenzi mema ya Baba, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwamba angenituma kuhubiri Injili na kuwaongoza kondoo Wake. Mungu ambariki na, milele, hilo Jina kuu! Nitadumu na Biblia Yake, nitumbukie au nizame, niwe maarufu au nisiwe maarufu. Kama mtu yeyote ananipenda, au la, nitampendeza Yeye. Nataka kufanya yale yanayompendeza Yeye.

160 Kama Baptisti wakinikataa, Methodisti; Pentekoste, juu ya "ushahidi wao wa kwanza, kunena kwa lugha, kuwa ni Roho Mtakatifu." Hiyo ndiyo sababu sisi si Wapentekoste. Hatuamini kwamba kunena kwa lugha hukufanya ujazwe na Roho Mtakatifu, si zaidi ya vile tunavyoamini kuishi katika zizi kunaweza kukufanya uwe nguruwe. La, bwana. Sio zaidi ya tunavyoamini kuishi katika—katika ikulu kungekufanya kuwa mfalme. Hakukufanyi! Unaweza kuwa mtumishi. Unaona? Unaweza kuwa chochote. La, bwana.

161 Tunaamini kwamba unapokea Roho Mtakatifu kwa tukio fulani, si kwa dhana ya kiakili ya kubuni ya Maandiko, bali kwa tukio ambalo wewe peke yako unajua. Sasa, ukitaka kujua kama alikuwa ni Roho Mtakatifu, angalia jinsi maisha yako yanavyojiendeleza baada ya tukio hilo. Itakwambia ni aina gani ya roho iliyokuingia.

162 Huenda ukanena kwa lugha au usinene. Lakini kwa nini Wapentekoste wakafanya jambo la kutisha namna hiyo? Shikeni hilo. Kwa nini Wapentekoste walifanya hivyo? Kwa nini? Kwa sababu, hapo mwanzo, wakati Mungu alipoanza kurejesha kule nyuma, miaka arobaini iliyopita, kurudisha karama, mtu fulani alianza kunena kwa lugha. Na kunena kwa lugha ndiyo karama ndogo zaidi, kulingana na mafundisho ya Paulo, ya kundi zima la karama. "Karama iliyo ndogo kuliko zote, ni kunena kwa lugha." Na mara walipofanya hivyo, wote walisisimkwa na kuunda madhehebu, na kuliita Baraza Kuu, ambalo ni Assemblies of God.

163 Sasa, nimezungumza na baadhi ya watu wao walio bora sana, wanatheolojia wao walio bora zaidi, nao wanasema, "Ndugu Branham, unasema kweli. Lakini tufanye nini sasa? Kama tungepinga hilo, tungefukuzwa. Nalo kanisa letu lingefikiria nini kutuhusu? Wakati, tumewafundisha kwa miaka mingi, tumewafundisha kwa miaka mingi, kwamba, 'Ushahidi wa Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha.' Vipi kama tukiibadilisha sasa?" Hiyo ndiyo laana ya dhehebu.

Bwana asifiwe! Hatuna dhehebu. Jinsi tu Roho anavyoongoza, tunamchukua.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tukio la kibinafsi.

164 Nimeona watu wakinena kwa lugha. Nimeona wachawi na walozi. Mmishenari yeyote anajua vivyo hivyo, ambaye amewahi kushughulikia uchawi na mashetani. Nimewaona wakisimama na kunena kwa lugha, na kutupa uchafu nyuma ya vichwa vyao, na kujikata kwa mkuki, na kunena kwa lugha na kuzifasiri. Nanyi mnasema huyo ni Roho Mtakatifu? Hakika, sivyo. Ni ibilisi.

Yesu kamwe hakusema, "Kwa ndimi zao mtawatambua," lakini, "Kwa matunda yao mtawatambua." Na Waefeso 5:1 ilisema, kwamba, "Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, utu wema, saburi, upole, imani, kiasi." Hiyo ni kweli? Haya basi.

165 Sasa, kama wewe ni Mmethodisti, aina hizo za matunda zinakufuata, hata huna hasira ya haraka, ya kupigana na msumeno uvumao; kama una subira, kwa kuwa una upendo, na unamjali kila mtu; ikiwa upendo wako wa kwanza ni Kristo, wa pili ni mwenzako, acha wewe uwe wa tatu, kushuka namna hiyo; kama unaendelea, una uvumilivu, upole, saburi, imani.

"Jamani," unasema, "Roho wa Bwana yuko juu yangu. Na kuna uponyaji wa Kiungu. Roho Mtakatifu ni yeye yule leo hii."

166 Sasa, unasema, "Ngoja kidogo. Ninafundishwa katika kanisa la Kristo. Siku za miujiza zimepita." Una ibilisi. Hiyo ni kweli.

Unasema, "Vema, tunapaswa kubatizwa. Katika Biblia, hakuna kitu kama kubatizwa kwa jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.' Ninaliona sasa hivi. Liko katika Maandiko. Ni Jina la Bwana Yesu. Kila mahali, ni Jina la Bwana Yesu."

167 "Subiri kidogo, tutakufukuza utoke Assemblies." Ukikubaliana na jambo hilo, una roho ya uwongo ndani yako. Unasikiliza mafundisho ya uwongo, au nabii wa uwongo.

168 Sasa, tafuta tu mahali pamoja ambapo waliwahi kubatizwa, jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," nami nitajisalimisha kwako. Nitawaonyesha, kila mahali, walibatizwa katika Jina la Bwana Yesu. Sasa, nani yuko sahihi, Assemblies au Biblia?

169 Ukisema, "Naam, nimenyunyiziwa. Mungu asifiwe, huo ni mzuri sana kwangu vile vile. Huna elimu ya kutosha tu. Nakwambia, wanyunyizie. Je, inaleta tofauti gani, kumwagilia maji au kuzamisha ndani?"

Sijali jinsi—jinsi inavyoonekana. Biblia ilisema tubatizwe. Na *kubatiza* maana yake ni "kuzamishwa."

Unasema, "Inaleta tofauti gani?"

170 Naam, vipi kama—kama Mungu alimwambia Musa, "Vua viatu vyako; uko mahali patakatifu"; Musa aseme, "Huko ni kujisumbua sana. Nitavua tu kofia yangu; ati inanibidi nifungue viatu vyangu"? Je, ingekuwa ni sawa vile vile? La, bwana. Mungu kamwe asingezungumza naye mpaka avue viatu vyake.

Na Mungu hatazungumza na kanisa mpaka litakaporudi kwenye masharti na kanuni ambazo Kristo aliziweka, wala halitawaliwi na mihemko fulani au madhehebu fulani kulivuta *huku* na *huko*. Itawabidi warudie kuamini miujiza, kuamini ishara, kuamini Roho Mtakatifu, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, na mambo haya yote. Itawabidi kurudi kwenye Hilo, la sivyo Mungu hatazungumza nao. Hiyo ni kweli kabisa. Hapo ndipo kanisa lilipo.

171 Hiyo ndiyo sababu sisi si madhehebu. Hiyo ndiyo sababu hasa sisi si wa dhehebu. Tunaamini Biblia, halafu kuna mambo mengi Humo ambayo hatujui, mengi sana, lakini, tunasimama wazi, Bwana Yesu, lifunue tu Hilo.

Na tutatembea katika Nuru, ni Nuru nzuri,
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema
yanang'aa;
Tumulikie kote, mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Si Methodisti, Wabaptisti, Presbiteri, bali, Yesu, Nuru ya ulimwengu.

> Enyi watakatifu wote wa Nuru tangazeni,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu;
> Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Kila mtu, kwa namna ya ibada sasa.

> Tutatembea katika Nuru, ninii nzuri . . . (Hebu ishikilie kidogo, mnaona.)
> Inakuja ambapo umande wa rehema unang'aa;
> Tumulikie kote, mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

172 Je, si afadhali kuwa na Yesu na Neno Lake, kuliko kuwa na wazo la dhehebu lolote kulihusu? Ni wangapi wangependelea kuwa na Yesu na Neno Lake?

Sasa, tafuta mahali pamoja hapa ambapo Mungu aliwahi kuagiza madhehebu. Tafuta mahali pamoja alipowahi kumweka mhubiri mwanamke ama kumtawaza mmoja, katika Maandiko. Tafuta mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi kunyunyiziwa au kumwagiliwa. Tafuta mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, popote, ni chochote ila Jina la Yesu Kristo; sio "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Tafuta mahali ambapo mtu mmoja aliwahi kubatizwa kwa jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Njoo unionyeshe. Ambapo, kila mtu alibatizwa katika Jina la Yesu.

173 Sasa tunaingia katika mambo ya kilindi kuliko haya sasa. Sasa tunaingia kwenye "ushahidi wa awali," na kadhalika, na kuona tu mahali ulipo.

Sasa, kama wakifundisha kinyume na hayo, wanafundisha mambo ambayo hayapo katika Biblia.

174 Kumbukeni, ninawaomba mahali pamoja palipowahi kuwa na madhehebu. Nionyeshe pamoja tu. Basi mtu fulani amekosea. Siombi kuwe na mmoja *hapa* na mmoja *hapa*, labda, kama huyo mwingine hakuwa. Ninawaonyesha. Nionyesheni mahali pamoja palipowahi kuwa na dhehebu, miaka mia tatu baada ya kifo cha mtume wa mwisho. Nionyeshe ambapo kuna dhehebu moja lisiloanzishwa na kanisa Katoliki. Nionyeshe mahali pamoja ambapo Biblia hailaani madhehebu. Basi kwa nini nyinyi ni dhehebu?

175 Nionyeshe mahali pamoja, sasa, mahali pamoja, mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi kunyunyiziwa, kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao. Simaanishi moja tu *hapa* na *pale*. Sasa nionyeshe mahali pamoja katika Maandiko yote. Nionyeshe mahali pamoja katika Maandiko yote ambapo mtu yeyote aliwahi kumwagiliwa, kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao. Nionyeshe mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi

kubatizwa katika jina la Ye-. . .Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mahali pamoja tu, mtu mmoja, ambapo mtu mmoja aliwahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

Nionyeshe mahali pamoja ambapo Mungu aliwahi kumweka mhubiri mwanamke kanisani, ama labda alisema awepo. Pako wapi?

Hiyo ni changamoto kubwa. Lakini nataka kupata swali lako, sasa, limewekwa mimbarani, kunionyesha lilipo mojawapo ya mambo haya; usiku wa leo, nitaomba msamaha. Ikiwa halipo, basi ikiwa hujatimiza masharti haya, basi kwa nini usiyatimize? Njoo uwe mmoja wetu. Ndivyo ulivyo, kwa vyovyote vile, kwa uwezekano.

176 Kama jina lako liko kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, utatembea katika Nuru, utaona Nuru. Mungu atalifunua, nawe utatembea ndani Yake. Hiyo ni kweli kabisa. Unaona?

177 Sasa nini? Siwarudishi kwenye kanisa. Ninawarudisha kwenye Biblia. Sasa, Paulo alisema nini? Paulo alisema nini? "Malaika kutoka Mbinguni akihubiri kitu kingine chochote isipokuwa *Hili*, na alaaniwe."

178 Mungu alisema, "Neno la kila mtu na liwe uwongo, na Langu liwe Kweli." Kwa hiyo sijali kanisa lolote linasema nini, Pentekoste, Baptisti, Presbiteri. Neno la Mungu ni Kweli. Kwa nini walianzisha hili? Kwa sababu ya madhehebu.

179 Pentecostal Assemblies of God, leo, wangetoa chochote, ndani kabisa ya mioyo ya hao walimu wakuu, kama kamwe hawakuanzisha fundisho hilo la sharti la "ushahidi wa awali: kunena kwa lugha." Wanajua hilo ni kosa. Halitastahimili kitu. Hakika halistahimili. Ninaweza kukuthibitishia kwa Biblia ya Mungu ya kwamba humpokei Roho Mtakatifu kwa kunena kwa lugha. Haipo Hapa. Loo, unafikiri; naam, hakika. Imeandikwa kwa uangalifu sana hata ingewadanganya walio Wateule. Mnaona?

"Ameificha kutoka kwa macho ya wenye hekima na busara, na kuifunua kwa watoto wachanga." Ni ufunuo wa kiroho. Hebu angalia ufunuo ukilipiga, na uone likiangaza. Unaona, haya basi. Unaona? Hilo hapo jambo unalohitaji kuliangalia, rafiki, unaona, liko hapo.

180 Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu ambaye ni Mwalimu wetu. Na Yeye haendi tu na kupata maskini mawazo ya kale ya uwongo, na kuyaleta hapa na kusema "Loo, haleluya! Hili hapa, kweli, limeandikwa papa hapa. Haleluya!" Roho Mtakatifu hurudi nyuma na kukuleta moja kwa moja kupitia katika Maandiko, anamweka moja kwa moja chini, moja kwa moja kupitia Maandiko. Mnaona? Hapo ndipo unapata Ukweli. Hivyo ndivyo hasa. "Kwa maana amri lazima iwe juu ya amri juu

ya amri, na kanuni juu ya kanuni juu ya kanuni." Hivyo ndivyo Biblia ilisema lifanywe.

181 Unasema, "Je, unalaani dhehebu?" La, bwana. "Je, unalaani wanawake wahubiri?" La, bwana. "Je, unalaani kunena kwa lugha?" La, bwana. "Je, unawahukumu watu hawa wanaobatizwa kwa jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu'?" La, bwana. La, bwana. Lakini, nasema, kama wanajua vizuri zaidi sasa, Mungu atawawajibisha wasipoifuata Nuru. Huenda hukulijua mpaka sasa hivi, lakini unalijua tangu sasa. Unaona?

Sasa, kama hufikirii ni kweli, chunguza Maandiko. Basi tafuta mahali pako, na urudi na kuliweka juu ya dawati hili usiku wa leo, nasi tutaona kama ni kweli au la. Ndipo uende ukalichunguze, kwa nia wazi, moyo wazi.

182 Sasa, hayo, sasa, mafundisho kama haya ni kwa ajili ya Maskani ya Branham, mnaona, hapa tu, papa hapa tu. Hakuna...

183 Laiti isingekuwa ni "Maskani ya Branham." Laiti ingeitwa tu "Maskani," hata haikuambatanishwa na jina langu.

184 Ninajiandaa kuligeuza kanisa hili...Nyote mnajua, tulipoinunua, niliinunua wakati nikifanya kazi kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma. Na kujenga kitu hiki hapa, na kukiita tu hivyo kwa sababu kwamba Ndugu Seward na hao wengine waliambatanisha jina langu nalo walipoliweka kwenye hatimiliki kule chini. Mara tu ninapoweza kumalizia jambo hili ambalo tuko ndani yake sasa, kanisa hili litapewa hii, jumuiya, na kutolewa tu; jina langu litaondolewa kwake.

185 Sidhani jina langu linapaswa kuwa kwenye kanisa hilo. Haipaswi kuwa "Maskani ya Branham." Inapaswa kuwa kanisa tu, "Kanisa la Bwana Yesu Kristo," au kitu kama hicho. "Maskani ya Bwana," mnaona, "Mahali pa kuishi," "Nyumba ya sala," au kitu kingine, ipewe jina la aina fulani. Acha kusanyiko lichague jina lao. Jina langu, mi—mimi ni mwanadamu tu. Jina langu halistahili kuwa kwenye hii, si zaidi ya chochote. Sababu ilibidi kuweka jina langu juu ya hili, ni kwa sababu jina langu lilikuwa kwenye hatimiliki, iliyosema, "Billy Branham." Mnaona? Na halipaswi kuwa hapo. La, bwana. Linapaswa kuwa kanisa la jumuiya. Hii, hii inapaswa kuwa kwa ku—kusanyiko hapa.

186 Na kanisa hili ni huru. Hakuna halmashauri ya wadhamini ama mashemasi watakaowaambia la kufanya. Kanisa hili, kwa kura nzima, linakwambia la kufanya. Hiyo ni kweli kabisa, ikiwa kuna uamuzi.

187 Kama hamumpendi mchungaji wenu, na kuna watu wawili au watatu wanapata jambo dhidi ya mchungaji, hawawezi kusimama pamoja na mashemasi wao, wadhamini, wao ni afisa tu walio hapa. Wana kura moja tu. Hivyo tu. Ikiwa yeye ni mchungaji msaidizi, ana kura moja tu. Yeye ni kama tu mlei

wa kawaida anayeketi kule nyuma. Kura nzima ya kanisa inasuluhisha hilo suala. Na hiyo ni kweli. Hiyo ni—hiyo ni kweli. Hakuna halmashauri ya mashemasi inayomtoa mchungaji, ama hakuna mchungaji anayeiondoa halmashauri ya mashemasi. Kanisa hufanya hivyo, katika kura ya jumla ya hilo jambo zima.

188 Ni huru lenyewe. Hatuna maaskofu. Hatuna waangalizi wakuu. Tunaye Yesu. Amina! Yeye ni Askofu. Yeye ni Mwangalizi Mkuu. Yeye ni Mchungaji Mkuu. Yeye ni Mfalme. Yeye ni Bwana. Yeye ndiye Mponyaji. Yeye ni Yote kwa Yote. Nasi ni raia Wake tu, tukitembea katika Nuru. Amina.

189 "Naye aliwaweka wengine Kanisani." Ati nini? "Kanisani," katika Mwili. "Akaweka wengine humo." Ati nini?

"Kwanza mitume," hao ni wamishenari. Tunaye mmoja hapa kanisani sasa, mvulana mdogo anayeketi kule nyuma, rafiki yangu, ndugu, ninamwita Creech Jefferies. Huo ndio wito wa kwanza, wa juu zaidi, mmishenari. Unasema, "Ati mtume ni mmishenari?" Kabisa. Nenda kaangalie katika kamusi na ujue *mtume* maana yake nini; maana yake, "mtu aliyetumwa." Nenda ukaangalie, maana ya *mmishenari*, "mtu aliyetumwa." Jambo lile lile. Wadhifa wa juu kabisa ni mmishenari anayesafiri baharini kwa ajili ya Bwana Yesu. Juu, "Kwanza ni mitume."

190 "Pili, manabii." Nabii ni nini? Mwonaji. Sio mtu anayejifanya . . .

Si mtume anayejifanya kuwa mmishenari na kukaa nyumbani, bali yule ambaye kwa kweli ni mmishenari.

Na nabii, mwonaji.

191 Mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, wachungaji, hao ndio walioko kwenye Mwili.

Katika mwili huo wa mahali hapo, basi, kuna karama tisa za kiroho. Mojawapo ni hekima, maarifa, uponyaji wa Kiungu, kunena kwa lugha, tafsiri ya lugha, karama hizi zote mbali mbali zilizo katika mwili wa mahali hapo.

Na hawa mitume, wachungaji, waalimu, na wainjilisti, wote wako hapa kuhakikisha kwamba, katika karama hizi, mambo haya yanafanya kazi sawasawa. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Wakipata jambo la uongo linazuka, upesi wanalilaani, maana si kulingana na Maandiko.

Acha mtu aje hapa juu, aseme, "Mungu asifiwe, nina mafuta mikononi mwangu. Tazama *hapa*. Mnajua, ni—ni—ninaamini nina Roho Mtakatifu, nami nina mafuta mikononi mwangu."

192 Utasikia mtu fulani akisema, "Hilo si la Kimaandiko." Hiyo ni kweli. "Hebu tuchukue na tuingie humu chumbani. Hebu tuyachunguze Maandiko kweli kweli. Nionyeshe katika Maandiko mahali hapo palipo, ushahidi wa Roho Mtakatifu."

193 Mmoja akasema, "Loo, nilinena kwa lugha. Nimempata."

"Nionyeshe katika Maandiko huo ndio ushahidi wa Roho Mtakatifu." Hiyo ni kweli.

194 "Loo, Bwana aliniita kuhubiri," anasema mwanamke fulani.

"Nionyeshe katika Maandiko alifanya hivyo." Naam.

195 "Loo, najua Bwana aliniambia. Alinibariki usiku ule niliobatizwa kwa jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.'"

"Nionyeshe katika Maandiko mahali unapopaswa kufanya hivyo."

196 "Vema, mimi ni mzuri tu kama mtu mwingine yeyote, nami ni Mmethodisti, ama Mbaptisti, ama Mpresbiteri. Mimi ni Mpentekoste."

"Nionyeshe katika Maandiko ambapo Mungu alisema jambo hilo." Mnaona? Hiyo ni kweli. Hamna.

197 Sasa, kuna changamoto kubwa kwenu ninyi washiriki wa maskani hii. Kuna changamoto kubwa sana. Sasa, ukipata jambo moja unalofikiri kwamba si sahihi, ambalo nimesema asubuhi ya leo, jambo moja ambalo ni kinyume na Maandiko, unawajibika kuliweka hilo kwenye mimbara hii jioni ya leo. Hiyo ni kweli. Wewe lilete na kuliweka hapa. Nionyeshe Maandiko, kifungu katika Biblia ambapo palikuwa na madhehebu, ya kwamba Yesu aliunda dhehebu, au mojawapo ya mambo haya ambayo nimefundisha. Ambapo aliwahi kumtawaza na kumweka mwanamke kanisani, kama mhubiri; ambapo aliwahi kuamuru kunyunyizia, kumwagilia; au—au kitu chochote cha aina hiyo ambacho nimekuwa nikizungumzia. Kiweke hapa.

Ndipo, usiku wa leo, tunaingia, Bwana akipenda, kwa "ubatizo wa Roho Mtakatifu," na katika "uzao wa nyoka, na wa mwanamke." Vema. Bwana awabariki. Ni wangapi wanaojisikia vizuri?

> Loo, najisikia kuendelea na safari,
> Loo, najisikia kuendelea na safiri;

Sasa mwimbieni Bwana huo kwa utamu sana.

> . . . Makao ya mbinguni ni maangavu na mazuri,
> Nami najisikia kuendelea na safari.
>
> Loo, najisikia kuendelea na safari, (Kuendelea na safari!)
> Loo, najisikia kuedelea na safari; (Kuendelea na safari!)
> Makao yangu ya Mbinguni ni maangavu na mazuri,
> Nami najisikia kuendelea na safari.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

198 Sasa, kumekuwa na jambo moja tangu nimekuwa kwenye kipindi hiki cha mapumziko kwa wiki hizi chache, niligundua,

hiyo imekuwa shida yangu. Nami nataka kukiri hilo sasa kwa kanisa langu. Niliketi nyuma ya ile miti ya mialoni na mihikori, hapa chini nikisoma, "Nilifanyia wapi kosa langu la kwanza? Ni nini kilinifanya nikosee? Ilikuwa ni nini?" Mnajua nilichogundua ambacho hunifanya nikosee? Kuna kitu kama kuvuka mpaka na kitu fulani. Je, mlijua hilo? Unaweza kujaribu kuwa sawa, na kujaribu kuwa mwema, na kisha unaweza kuwa mwema kupindukia. Nami nimewaacha tu watu wanisukume pande zote. Mnaona?

Watasema, "Vema, Ndugu Branham, njoo huku. Bwana aliniambia nikuambie hivi."

"Vema, sawa, ndugu, mimi huyu hapa naja."

"Loo, Ndugu Branham, usiende *kule*, *huku*."

199 "Vema, labda afadhali nisiende huko." Mnaona? Wala hujui la kufanya. Hilo ndilo linalonifanya kushikwa na wasiwasi.

Ninaenda mahali ambapo Bwana ananiongoza kwenda, wala sijali mtu yeyote anasema nini kulihusu. Mnaona? Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hivyo, sitaumiza hisia.

200 Halafu nikaona jambo lingine. Watoto wangu huko juu wamekuwa kundi la vichaa, wakipiga mayowe usiku, na kadhalika, watu wakilundikana ndani na nje ya nyumba pale, wakati wote, watu wakija kutoka kila mahali. Siwalaumu watu kutokana na hilo, wagonjwa. Lakini tumepanga yote hayo.

Na hapa kanisani, ninapokuja kufanya mkutano, mbona, karibu inanibidi nitoke nje, nitoke nje ya kanisa, kwa maana watu wanashikilia tu, na *hili* na *lile*. Nimechoka sana, na wakati mwingine nikitoka kwenye ibada ya uponyaji, nami si mzuri sana kwao, nasema . . .

"Aisee, Ndugu Branham, Bwana alisema . . . "

"Naam. Tunapokuja hapa, tunaenda . . . " Hilo si jema. Sipaswi kufanya hivyo. Haitupasi kufanya hivyo.

201 Sasa tumefanya mipango ya kushughulikia hilo. Na sasa, kumbukeni tu, mtu yeyote anayetaka . . . Nataka kuona kila mtu. Na ninataka kuwa na wakati, na kuzungumza na watu. Kwa njia hii, huwezi. Unamleta mtu fulani mle ndani, na, muda si muda wajua, muda wako wote umepotelea kwa mmoja, na—na huwezi kumwona huyo mwingine. Na hiyo si sawa. Watu hutoka mbali, wapate kusema nawe maneno machache tu. Na ikiwa Mungu ame—amewapa watu hao imani hiyo kwangu, kuamini hivyo, wanastahili muda kidogo wa kufundishwa. Hupaswi kuwafukuza tu, kusema, "La, simwoni mtu yeyote." Hiyo si sawa. Kwa sababu, ninaogopa kufanya hivyo, maana . . .

Mtu anakuja na kusema, "Sasa, Bwana ananiambia, Ndugu Branham, ya kwamba unapaswa kufanya jambo *fulani*, *fulani*. Haya ni—haya ni mapenzi ya Bwana sasa." Bwana ataniambia mapenzi Yake. Mnaona?

202 Bw. King, ni wangapi wanamkumbuka R. A. King, alikuwa akija hapa, alikuwa hapa chini? Alisema. . . Nilikuwa nikijenga mashua kule juu, siku moja. Akasema, "Sasa, Ndugu Branham, wewe jenga mashua hiyo kulingana na maelezo yako mwenyewe."

203 Kasema, "Nilikuwa najenga. . . Ama, mtu fulani alikuwa akijenga mashua wakati mmoja, ndipo jamaa mmoja akaja hapo, kasema, 'Unapaswa kukata kingo hizi *hivi*.' Vema, akajaribu hivyo. Mwingine akasema, 'Loo, unapaswa kufanya *hivi*, kila kitu, mba—mbavu na kila kitu. Mashua inapaswa kuwa *hivi*, na gubeti iwe *hivi*, na kichwa, na shetri, na u—usukani.'"

204 Naye akasema, "Ilikuwa ni kitu cha kuchukiza sana ulichopata kuona, alipomaliza." Kasema, "Alichukua tu hiyo mashua na kuipakia nyuma ya nyumba. Ndipo akaanza na misumeno yake, akijikatia nyingine."

205 Kasema, "Mtu akaja hapo na kusema, 'Aisee, *hivi* ndivyo unavyopaswa kuijenga.' Kasema, 'Ile, iliyojengwa na maagizo ya wengine, iko huko nje kwenye uwanja wa nyuma. Ninaijenga hii kulingana na vile ninavyofikiri inafaa kujengwa.'" Hiyo ni kweli.

206 Sasa, Mungu, kama anataka nifanye chochote, ataniambia la kufanya. Kama unafikiri kwamba nimekosea katika kile ninachofanya, ama chochote kama hicho, wewe niombee, kwamba Mungu atanisahihisha. Unaona? Maana siwezi kusikiliza mengi kupindukia.

207 Sasa, wewe hapa labda kanisani, inakupasa tu kusikiliza labda mtu mmoja au wawili, lakini hapa ninaingia kwenye makumi ya maelfu. Ninawezaje kufanya hivyo? Ndipo nikasema, "Kabla sijamjibu mtu yeyote, nitakaa chini na kulichunguza vizuri, nione Roho Mtakatifu anaelekeza wapi. Kisha nitamwambia mwanamume ama mwanamke huyo, yeyote yule, na huo ndio uamuzi wangu. Nitaushikilia. Hiyo ni kweli, kaa papo hapo."

208 Sasa, mahojiano yamepangwa. Mtu yeyote anayetaka kuniona, sawa kabisa, ikiwa utapiga simu kwa BUtler 2-1519. Angalia tu katika kitabu cha orodha ya simu na utafute William Branham, BUtler 2-1519, mipango itafanywa kwa mahojiano. [Nambari ya simu imebadilika—Mh.] Itaandikwa, wakati hasa na mahali pa kufanyiwa. Na ninaweza kukutana na kila mtu, kuonana nao, kuwasaidia kwa shida zao na kadhalika. Lakini siwezi kuingia tu na kukaa siku moja na mmoja, na saa nne au tano na *huyu*, na kesho yake nikose kitu hicho chote. Tuna muda *kiasi* fulani. Tunawauliza wanachotaka, na muda gani, na kuileta chini moja kwa moja. Na tunaona kila mtu. Tunayo hiyo.

209 Na mtu atakayejibu simu atakuwa ni Bw. Mercier hapa, ama Bw. Goad, anayeketi pale pale. Nao wataandika hilo kwenye

kitabu changu, haswa, kwa mahojiano, nami nitamwona kila mtu.

210 Kama ni jambo maalum, ikiwa ni wakati wa ibada ya maombi sasa, kwa ajili ya wagonjwa, leteni wagonjwa wenu na wanaoteseka ndani na waache wasikilize siku moja ama mbili usiku, sasa. Tutawaombea kwa ajili ya magonjwa ya dharura.

211 Lakini basi, baada ya kama siku kadhaa usiku, ninataka kuanza huduma yangu mpya, na ninataka kuwarudisha hapa katika chumba hiki. Kwa sababu, mnajua hilo ono. Ni wangapi wanaokumbuka hilo ono? Hakika, mnakumbuka. La lile hema dogo chumbani.

212 Sasa, nitamchukua Meda pamoja nami, katika usiku wa kwanza, kwa sababu ya kuwapeleka ndani wanawake. Na kisha ikiwa . . . Nione jinsi inavyofanya kazi nikiwa pamoja naye tu humo ndani. Na basi kama haifanyi kazi vizuri, kwa njia hiyo, basi nitageuka na kutuma wanawake wawili kwa wakati mmoja, kuleta wanawake wawili kwa wakati mmoja, maana wanaingia mahali ambapo ni mwanamume tu. Mnaona? Na kwamba, bila shaka, tuna nia safi. Lakini ibilisi hayuko nayo huko nje, mnaona, kile ambacho angefikiria juu yake, mnaona, na kile ambacho ulimwengu ungesema.

Lakini ni huduma ambayo siwezi kuifahamisha umma. Hakuna mtu atakayeiga hii. Unaona? La, bwana. La. Najua iko ukingoni sasa hivi. Ninaweza kuonekana kama tu kunyosha mkono huko na kuishika. Imekaa pale pale.

213 Jana usiku nilikuwa nikiota kabla tu sijaamka asubuhi ya leo, Ndugu Neville. Ni—nilikuwa nikiota ndoto. Na nilifikiria huduma . . . Sijui nilichokuwa nikifanya. Lakini, chochote kile, loo, unazungumzia kuhusu mambo yanayotukia, sijawahi kuona kama hayo. Niliamka nikilia tu, nikisifu. Nilimgonga mke wangu usoni kwa mkono wangu namna *hiyo*—namna *hiyo*, nikimsifu Mungu tu, nimelala pale.

Loo, na—najua tu ya kwamba kuna kitu papa hapa kilicho tayari kufikiwa na kushikwa. Kitakuwa kikubwa zaidi kuliko kilivyowahi kuwa. Itakuwa ajabu. Ninaamini Mungu anajitayarisha kufanya jambo kubwa. Lakini sasa hatuna budi kuliendea kwa uaminifu, kwa akili, na moja kwa moja katika Neno la Mungu. Sahihi. Loo, tunampenda.

214 Sasa kumbukeni, kama rafiki yako yeyote au mtu yeyote anataka kuniona na anataka kuongea nami kuhusu jambo dogo ambalo ni la faragha, acha wapige simu BUtler 2-1519 na kutakuwa na mahojiano yatapangwa mahali hapo. [Nambari ya simu imebadilika—Mh.] Siwezi kuwa nao nyumbani kule, na karibu na maskanini, maana mnaingia humu ndani . . .

Ninapitiliza muda sana nikihubiri. Nami nakaa hapa, kwa sababu siko pamoja nanyi sana. Nami ninawashikilia tu kadiri niwezavyo, ili kuingiza kila Neno ndani. Kwa sababu, marafiki,

huu ndio wakati pekee ambao itatubidi kufanya hivi. Haya yote yatakwisha, hivi karibuni. Tunashuka moja kwa moja kwenye bonde, kushuka moja kwa moja. Waangalie wale ambao wamesalia tangu mwaka jana, ambao wamekuwa hapa. Mnaona? Kwa hivyo tunashuka kwenye bonde. Tunapaswa kufanya hivi sasa. Hii inabidi ifanyike sasa. Na, sasa, hiyo ndiyo sababu ninawashikilia.

215 Unasema, "Vema, hilo, vipi kuhusu Maandiko ya hilo?"

Naam, Paulo alihubiri usiku kucha, usiku mmoja. Ndipo mtu akaanguka nje ya jengo, akafa. Ni wangapi wanajua hilo? Usiku kucha! Paulo akamwendea na kuulaza mwili wake juu yake, akamshika, moyo wake ukaanza kudunda pamoja na moyo wa jamaa huyo, kasema, "La, yeye . . ."

58-0928M Ubatizo Wa Roho Mtakatifu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org